Njia na Uzoefu wa Watoto na Vijana Ambao Wanajihusisha na Kazi za Mikono na Uchimbaji Mdogomdogo wa Dhahabu nchini Tanzania

Mradi wa USAID Kizazi Kipya

Novemba 2017

USAID FROM THE AMERICAN PEOPLE

pact building local promise.

IFAKARA HEALTH INSTITUTE

Mradi wa USAID Kizazi Kipya una lengo la kuwawezesha yatima wengi zaidi wa Kitanzania na watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi- watoto, na vijana wadogo walioko kwenye vituo vya watoto yatima na ambao wako katika mazingira hatarishi ya kupata maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na matatizo mengine - kutumia huduma sahihi zinazohusiana na VVU na UKIMWI na zingine kwa ajili ya kuboresha huduma, afya, lishe, elimu, ulinzi, kazi, na afya ya kisaikolojia.

Pact ni ahadi ya kesho bora kwa jamii ambazo zinakabiliwa na umasikini na kutengwa. Tunahudumia jamii hizi kwa sababu tunataka kuwa na ulimwengu ambapo kila mtu anamiliki mustakabali wake. Kwa kufanya hivyo, tunajenga utaratibu wa ufumbuzi kwa kushirikiana na mashirika ya ndani, biashara, na serikali zinazojenga jamii endelevu na yenye ujasiri ambapo wale tunaowahudumia wanasikika, wanakuwa na uwezo na wenye nguvu. Kiuhalisia karibia nchi 40, mbinu ya kuunganisha ya Pact imetengeneza mustakabali wa maendeleo ya kimataifa. Tutembelee kupitia www.pactworld.org.

Novemba 2017

Kanusho:

Ripoti hii imeweza kuandaliwa kwa msaada wa watu wa Marekani kupitia Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID) chini ya masharti ya makubaliano ya ushirika Namba. AID-621-A-16-00001. Yaliyomo ni wajibu wa Pact na wabia wake wote wa mradi na siyo lazima kuwa na mitazamo ya USAID au Serikali ya Marekani.

Picha ni mali ya Mradi wa USAID Kizazi Kipya na hazirusihiwi kutumika bila idhini. Picha ya kwenye jalada la juu ni ya wazazi na watoto wao wakichenjua dhahabu.

Marejeo:

Metta, E., A. Ramadhani, and E. Geubbels. 2017. *Pathways and Experiences of Children and Adolescents Who Engage in Artisanal and Small-Scale Gold Mining-Related Activities in Tanzania*. Dar es Salaam, Tanzania: Pact and Ifakara Health Institute.

Shukrani:

Ripoti hii imeandikwa na Emmy Metta, Ramadhani Abdul, na Eveline Geubbels wa Taasisi ya Afya Ifakara. Fedha kwa ajili ya shughuli za utafiti zilitolewa na USAID kupitia mradi wa USAID Kizazi Kipya, na kusimamiwa na Pact.

Waandishi wanapenda kushukuru kwa msaada wa kitalaam na usafiri uliotolewa na Ofisi ya Pact Tanzania na wasimamizi na wafanyakazi wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini. Tunashukuru serikali za mitaa katika wilaya tatu za Chunya katika mkoa wa Mbeya, Songwe katika mkoa wa Songwe, na Bukombe katika mkoa wa Geita kwa msaada wao na kutoa idhini ya kufanya utafiti na kutusaidia kupata maeneo kwa ajili ya utafiti wetu. Katika maeneo ya utafiti, shukrani zetu za dhati ziende kwa maafisa watendaji wa kata na kijiji kwa msaada wao usio na kikomo katika kutambua washiriki wetu wa utafiti. Shukrani zetu za pekee pia ziende kwa wasaidizi wa utafiti waliosaidia shughuli za kukusanya taarifa na kuziandaa. Tunawashukuru sana washiriki wa utafiti kwa utayari wao wa kuzungumza na kubadilishana uzoefu wao na watafiti.

Yaliyomo

Vifupisho i
Muhtasari Jumuishi ii
1. **Utangulizi** 1
1.1. Kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo 1
1.1.1. Uchimbaji rasmi/halali 1
1.1.2. Uchimbaji usio rasmi/haramu 2
1.2. Watoto walioko kwenye machimbo ya madini 2
1.3. Mfumo wa taifa wa kisheria 3
1.4. Mwitiko wa kitaifa 3
1.5. Mradi wa USAID Kizazi Kipya 3
1.6. Malengo ya utafiti 5
2. Mbinu ya Utafiti 6
2.1. Maeneo ya utafiti 6
2.2. Muundo wa Utafiti 6
2.2.1. Majadiliano ya kikundi na wanajamii wa kawaida 6
2.2.2. Mahojiano ya watu muhimu 7
2.2.3. Mahojiano ya Kina 7
2.3. Ukusanyaji taarifa na uchambuzi 8
2.3.1. Miongozo ya ukusanyaji taarifa za majaribio 8
2.3.2. Ukusanyaji taarifa halisi 9
2.3.3. Uchambuzi wa taarifa na uthibitishaji 9
2.4. Masuala ya kimaadili 10
3. Matokeo ya Utafiti 11
3.1. Wadau 11
3.2. Mtoto ni nani kwa mujibu wa jamii 11
3.3. Haki na majukumu yanayojulikana ya watoto 12
3.4. Mitazamo ya jamii kuhusu ajira za watoto 13
3.5. Je wachimbaji watoto ni kina nani? 14
3.5.1. Takwimu 14
3.5.2. Kusoma 16
3.6. Sababu na mazingira ya ajira za watoto kwenye migodi 17
3.6.1. Sababu kuu: Umaskini wa kaya 17
3.6.2. Talaka na ndoa kuvunjika 18
3.6.3. Elimu kupewa kipaumbele kidogo 18
3.6.4. Mazingira ya kijamii ya watoto 18
3.6.5. Wazazi kuwa mbali na watoto wao kwa muda mrefu 20
3.6.6. Msukumo kutoka kwa wenzao 20
3.7. Wachimbaji watoto wanatokea wapi 21
3.8. Wachimbaji watoto hukaa wapi 22
3.9. Utaratibu wa usalama na kushiriki katika kazi za uchimbaji madini 22
3.9.1. Aina za kazi ambazo wachimbaji watoto hufanya 22
3.9.2. Kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika shughuli za uchimbaji madini 23
3.9.3. Watoto wachimbaji hufanya kazi kwa muda gani 24
3.9.4. Jinsi wachimbaji watoto wanavyopata kazi migodini 25
3.10. Malipo ya kufanya kazi migodini 26
3.10.1. Jinsi wachimbaji watoto wanavyolipwa 26
3.10.2. Kuamua jinsi ya kutumia mapato 27
3.11. Sababu za waajiri kuajiri watoto 28
3.12. Hatari zinazohusiana na kufanya kazi kwenye migodi 29
3.12.1. Hatari za kiafya 29
3.12.2. Hatari za kijamii 31
3.12.3. Ukatili na unyanyasaji wa kijinsia 31
3.13. Uwepo na upatikanaji wa huduma katika maeneo ya migodi 32
3.13.1. Upatikanaji wa shule 32
3.13.2. Upatikanaji wa huduma za afya 33
3.13.3. Mitazamo kuhusu VVU/UKIMWI na upimaji wa VVU na matibabu 34

3.14. Mipango/miundo iliyopo kwa ajili ya kuwasaidia Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini 35
3.14.1. Kamati za elimu za kata 35
3.14.2. Sheria ndogo 36
3.14.3. Mipango ya ulinzi ya kifedha 36
3.14.4. Programu za ulinzi wa mtoto 37
4. Mapendekezo 39
4.1. Hatua ya 1: Mapendekezo ya utekelezaji 39
4.1.1. Jamii 39
4.1.2. Utoaji wa huduma 39
4.1.3. Sera 41
4.2. Hatua ya 2: Mapendekezo ya wazazi na wajumbe wa kamati ya maendeleo ya Kata kwa ajili ya shughuli za kuimarisha uchumi 41

Vifupisho

UKIMWI	upungufu wa kinga mwilini
ALWHIV	vijana wanaoishi na virusi vya UKIMWI
ART	Dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI
ASM	kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo
CIM	watoto walioko kwenye machimbo ya madini
CSOs	asasi za kiraia
FGD	majadiliano ya kikundi
GEREMA	Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Geita
VVU	virusi vya ukimwi
IDI	mahojiano ya kina
ILO	Shirika la Kazi Duniani
KII	mahojiano na mtu muhimu
km	kilomita
LSM	uchimbaji mkubwa wa madini
MBEREMA	Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Mbeya
OVC	watoto yatima na wanaoishi kwenye mazingira hatarishi
STI	maambukizi kwa njia ya ngono
TASAF	Mfuko wa Maendeleo ya Jamii
USAID	Shirika la Marekani kwa ajili ya Maendeleo ya Kimatatifa
VSLA	Chama za kuweka na kukopa vijijini
WFCL	mazingira mabaya sana ya ajira kwa mtoto

Muhtasari Jumuishi

Usuli

Ripoti hii inatoa matokeo ya tathmini ili kubuni muundo wa wa huduma kwa kundi moja dogo maalum la walengwa chini ya mradi wa USAID Kizazi Kipya: watoto walioko kwenye machimbo ya madini (CIM). Ajira za watoto ni kinyume cha sheria nchini Tanzania, lakini watoto wapatao 31,000 wanafanya kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini (ASM), ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa madini ya dhahabu. Kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini zina sifa ya matumizi ya zana na mbinu duni na mapato madogo. Hatari za kiafya na kijamii kwa watoto wanaofanya kazi katika machimbo ya madini ni nyingi na kubwa na zinaweza kuwa na athari za muda mrefu kwenye afya na maendeleo yao.

Tathmini hii ilikuwa na malengo makuu mawili:

1. Kutathmini njia za ushiriki wa watoto katika shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini na tabia zinazojenga hali fulani katika jamii.
2. Kutumia matokeo ya utafiti kutoka lengo la 1 kuelezea mfano sahihi na halisi wa utekelezaji kwa ajili ya kuboresha afya na utoaji wa huduma za kijamii kwa watoto kwenye machimbo ya madini.

Taarifa zilikusanywa kupitia majadiliano ya kikundi (FGDs), mahojiano ya watu muhimu (KIIs), na mahojiano ya kina (IDIs) yalifanyika kwa kushirikisha jumla ya washiriki 164 kutoka wilaya ya Bukombe (Geita), Chunya (Mbeya), na Songwe (Songwe) kati ya mwezi Mei na Julai 2017. Washiriki walikuwa ni pamoja na watoto na vijana wanaofanya kazi katika machimbo ya madini, watoto wengine na vijana wanaoishi katika jamii za wachimbaji madini, wazazi/walezi wa watoto wachimbaji, walimu, wamiliki wa migodi, wasimamizi, viongozi wa serikali za mitaa, na wadau wengine. Uchambuzi wa matokeo ulijadiliwa na serikali na wadau washirika na kuwashirikisha wanajamii kwa ajili ya uthibitisho ili kusaidia kuandaa muundo wa utekelezaji.

Matokeo muhimu

- Katika maeneo ya utafiti kuna mchanganyiko wa wachimbaji wadogowadogo walio rasmi na wasio rasmi, wadau mbali mbali wanapatikana katika maeneo hayo kuanzia kwa wale wanaomiliki mashimo ya migodi au maeneo ya uchakataji mawe, wale wanaomiliki na kutoa huduma karibu na maeneo ya migodi, mpaka kwa vibarua watoto na watu wazima na familia zao. Hata hivyo, mtu yeyote mwenye gunia la mawe yenye madini anaweza kuchukuliwa kama mchimbaji na mwajiri wa watoto.

- Jamii za wachimbaji madini zinatafsiri mtoto kwa kuangalia uhuru wa kiuchumi kuliko umri au kuwa sehemu ya muundo wa familia.

- Kuna maoni mengi kwamba wazazi wanawajibika kuwajali na kuwahudumia watoto wao, kwamba watoto wana haki ya kwenda shule, na kwamba ajira kwa mtoto hususan ya kufanya kazi ngumu mbali na kazi ndogondogo ya kusaidia kaya haipaswi kupuuzwa.

- Sababu kuu zilizotajwa za watoto kufanya kazi katika machimbo ya madini na kutokuwepo shuleni zilikuwa ni umasikini wa kaya unaosababishwa na viwango vya juu vya kuvunjika kwa ndoa na kipato duni kinachotokana na uchimbaji madini usio na muundo thabiti, kutoa kipaumbele kidogo kwenye elimu kwa sababu ya makazi ya muda mfupi na ya kuhamahama katika maeneo ya machimbo ya madini, ushawishi rika, mazingira ya kijamii na mfumo wa maisha unaomfanya mtu kujiingiza kwenye uchimbaji madini, tamaa ya kupata fedha za haraka, na usimamizi mdogo wa wazazi.

- Watoto wachimbaji wote wasichana na wavulana wanaripotiwa kuanza kufanya kazi katika migodi kuanzia umri wa miaka 7. Watoto wadogo zaidi kuliko hawa wanaongozana na mama zao. Watoto walioko kwenye machimbo ya madini hujumuisha yatima, watoto kutoka kwenye kaya zenye mzazi mmoja na wale wenye wazazi wote wawili hai.

- Kufanya kazi katika machimbo ya madini inasemekana kuwa ni sababu kuu ya kuacha shule, utoro, na kushuka kwa kiwango cha ufaulu cha shule.

- Muda wa kazi hutegemea kama watoto wanafanya kazi peke yao au na familia yao au mtu mwingine na muda unaweza kuwa mrefu sana.
- Malipo yanatofautiana sana. Watoto wanadhulumiwa kutokana na udhaifu wao wa kupatana bei. Wakati mwingine wanakubaliana lakini malipo yanachelewa au yasilipwe kabisa au wakipata madini wananyang'anywa.

- Matukio kadhaa na aina za unyanyasaji wa kijinsia na kimwili wa watoto yaliripotiwa kutoka kwenye maeneo yote ya utafiti.

- Matatizo ya kiafya ya watoto walioko kwenye machimbo ya madini yaliyoonekana na kuripotiwa yanaanzia kwenye yale maalum yatokanayo na shughuli za uchimbaji madini (majeraha, madhara ya zebaki na asidi ya sulfuriki), yanayohusiana na mazingira wanayoishi (ugonjwa wa tumbo na njia ya haja kubwa, malaria, nimonia/kichomi), na yanayohusiana na mazingira duni na hatari ya kijamii (VVU, unyanyasaji wa kingono/kimwili, madhara ya pombe na madawa ya kulevya).

- VVU inaonekana kuwa vya kawaida katika maeneo ya migodini, na tabia ya kujikinga iko chini. Huduma za VVU zinapatikana umbali wa kilomita 15 ndani ya machimbo, lakini umbali umekuwa ni kikwazo cha upatikanaji wa huduma hizo. Huduma hafifu za uhamasishaji au mifumo ya kujikinga, kupima, kuhudumia, na matibabu iliyopo katika maeneo hayo inaweza kuunganishwa na/kupanuliwa.

- Mifumo ya kijamii iliyopo ambayo mradi wa USAID Kizazi Kipya unaweza kufanya nayo kazi ni pamoja na kamati hai za elimu za kata, sheria ndogo za jamii dhidi ya ajira za watoto, vikundi vya kuweka na kukopa katika baadhi ya maeneo, mifuko midogo ya maendeleo ya watoto na vijana, ambayo ni asilimia 5 ya mapato ya halmashauri ya wilaya.

Mapendekezo muhimu

- Kuongeza uelewa kuhusu hatari za kiafya na maendeleo zinazohusiana na watoto wanaofanya kazi katika machimbo ya madini.
- Kuwezesha kuimarisha uchumi na vyanzo mbadala vya mapato kwa (familia za) watoto wanaofanya kazi kwenye machimbo ya madini, kupitia vikundi vya kuweka akiba na kukopesha, mafunzo ya ufundi, mtaji mdogo wa kuanzia, na mafunzo ya usimamizi binafsi wa fedha na ujasiriamali.
- Kutoa elimu ya malezi kwa wazazi ili kuwasaidia wazazi kuelewa madhara ya ajira za watoto walioko kwenye migodi, kusaidia familia kuendelea kuwa pamoja, na kupunguza ndoa za utotoni.
- Kusaidia uanzishaji wa vituo vya kuhudumia watoto ambao mama zao wanafanya kazi migodini.
- Kushirikisha jamii katika kutunga na/au kutekeleza sheria ndogo za ajira za watoto, k.m., kupitia kamati tendaji za kata.
- Kuwaunganisha watoto na vijana walionyanyaswa kingono au kimwili na huduma za kisheria na kijamii.
- Kuhimiza wazazi na jamii kusaidia watoto kuendelea na shule mpaka watakapohitimu masomo yao bila kikwazo. Kamati za maendeleo ya shule zinapaswa pia kuwajumuisha viongozi wa jamii, wadau wa madini, na wazazi wa wachimbaji watoto.
- Mazingira ya shule yanapaswa kuwavutia wanafunzi, kwa mfano kwa kuanzisha programu za michezo na kuimarisha mpango wa kutoa chakula shuleni ili kuwahimiza na kuwahamasisha wanafunzi kuwepo shuleni.
- Kutoa elimu endelevu ya afya kuhusu kinga na matibabu ya magonjwa ya kuambukiza, ikiwa ni pamoja na VVU na magonjwa mengine yanayoambukizwa kwa njia ya ngono (STIs), na kukabiliana na hatari maalum zinazotokana na uchimbaji madini. Programu kama vile usambazaji wa vyandarua zinapaswa pia kulenga jamii katika maeneo ya uchimbaji madini, na uboreshaji wa mifumo ya maji na usafi wa mazingira unapaswa kutiliwa maanani kwenye migodi.

- Huduma za kutembelea na kupima VVU, kutoa ushauri nasaha, utoaji wa dawa wa kufubaza virusi vya UKIMWI (ART) na/au msaada wa (elimu, usafiri, usindikizaji, kufuatilia) upataji wa huduma za VVU unapaswa kuimarishwa.
- Kuruhusu huduma za kupima VVU na kutoa ushauri kwa watoto waliobalehe/waliovunja ungo wenye umri wa chini ya miaka 18 bila idhini ya mzazi/mlezi.

1. Utangulizi

1.1. Kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo

Tofauti na uchimbaji mkubwa wa madini unaofanywa na viwanda, kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini hutumia zana na mbinu duni, mara nyingi hutumia mikono kuchimba, kusafirisha, kuchakata, na kuuza madini. Kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini mara nyingi huwa na athari mbaya za kimazingira na kijamii kwa sababu hufanyika katika mazingira duni ya kazi na hatari. Kwa sababu wachimbaji hawana rasilimali za kitaalam na ujuzi, ufanisi wa uzalishaji mara nyingi huwa ni mdogo, na kusababisha kupata faida ndogo. Hata hivyo, kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini ni njia muhimu ya kujipatia kipato kwa mamilioni ya wanaume na wanawake. Mapato yanayotokana na kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini yanaweza kuwa makubwa zaidi kuliko yale yaliyopatikana kutoka kwenye shughuli zingine na, ukilinganisha na baadhi ya shughuli zingine za kujiingizia kipato, kama vile kilimo, kinaweza kuwa chanzo cha haraka cha fedha.[1]

Kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini ulikuwa ndiyo uzalishaji mkubwa wa madini nchini Tanzania kati ya mwaka 1987 na 1997 na, licha ya ongezeko la uchimbaji mkubwa wa madini unaofanywa na viwanda, unaendelea kuwaingizia kipato muhimu watu katika jamii za wachimbaji madini. Utafiti wa Nguvu Kazi Jumuishi Tanzania[2] wa mwaka 2014 ulikadiria Watanzania wapatao 614,103 walikuwa wanafanya kazi katika machimbo ya madini na mawe, na wengi wao wakiwa katika ajira zisizo rasmi, ikiwa ni pamoja na watoto 30,827 wenye umri wa miaka 5-17. Kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini hufanyika nchini kote Tanzania, zikizalisha dhahabu, almasi, vito, bati, chumvi, chokaa, mawe ya asili yaliyochongwa, jasi, mchanga na changarawe. Shughuli za uchimbaji madini nchini Tanzania zinahusisha watu ambao hudhibiti mgodi, wamiliki wa mashimo (ambao hukodi mashimo kutoka kwa watu wanaodhibiti mgodi), wasimamizi, na wafanyakazi. Mbali na shughuli za madini za moja kwa moja, shughuli za huduma katika maeneo ya madini ni pamoja na maandalizi ya chakula na kuhudumia, burudani, na biashara ya ngono. Watoto wanahusika moja kwa moja katika shughuli zote mbili za uchimbaji madini na huduma.

Mwaka 2013, Pact ilifanya utafiti wa awali miongoni mwa wachimbaji watu wazima/wamiliki wa mashimo 849, wamiliki wa migodi 46, na wakuu wa kaya 647 katika vitalu vitatu vya madini ya dhahabu Tanzania (Chunya, Geita, na Tarime), ikizingatia takwimu za uzalishaji wa sasa, wastani wa mapato ya mtu mmoja mmoja na kaya za wachimbaji, na uthamini wa vifaa vya uchimbaji madini. Ilionesha kuwa wachimbaji madini wana viwango vidogo vya elimu, huku wanawake wakiwa na kiwango kidogo zaidi cha wastani wa elimu kuliko wanaume. Ilionekana kuwa wachimbaji wengi walikuwa wakifundishwa na wachimbaji wenzao katika maeneo ya machimbo ya madini. Uchimbaji wa madini ulikuwa ndiyo chanzo pekee cha kujiingizia kipato kwa asilimia 50 ya wachimbaji, na wengi hufanya kazi zaidi ya saa 13 kwa siku. Viwango vya uhaba wa chakula vilikuwa sawa kati ya kaya za wachimbaji madini na wasio wachimbaji madini, lakini kaya za wachimbaji madini zinatumia kiasi kikubwa zaidi cha mapato yao kugharamia huduma za afya. Ingawa hakuna taarifa za afya zilizokusanywa katika utafiti huu, wachimbaji wengi wa madini walisema wanatumia vifaa vya hatari, kama vile vilipuzi na zebaki, wakati wengine walisema wanatumia sianidi[3] (cyanide).

Ziara za tathmini zilizofanywa kwenye maeneo ya mradi wa USAID Kizazi Kipya zinaonesha kwamba kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini zinafanyika kisheria na kinyume cha sheria.

1.1.1. Uchimbaji rasmi/halali

Ili kufanya shughuli za uchimbaji madini kisheria, wachimbaji huomba leseni ya uchimbaji madini kutoka kwenye idara ya madini ya Mkoa ambayo ina jukumu la msingi la kudhibiti shughuli zote za uchimbaji madini kwenye mkoa husika na kutwaa leseni ya madini. Mfumo wa maombi ya Leseni ya Madini kwa njia ya Mtandao (The Online Mining Cadastre Transactional Portal), unaoendeshwa na idara ya madini ya mkoa, unafungua milango kwa umma ili kupata taarifa za leseni, kutuma maombi, na kufanya malipo. Mara baada ya waombaji kukamilisha mchakato wa maombi, uandaaji wa leseni ya madini huchukua siku 1-7.

[1] H. Poole Hahn, K. Hayes, and A. Kacapor. 2014. *Breaking the Chain: Ending the supply of child-mined minerals*. Washington, DC: Pact.

Kuna aina mbili za leseni ambazo wachimbaji wadogo wadogo wanaweza kupata: leseni ya uchimbaji madini ya msingi inayoweza kuongezwa muda kila mwaka na leseni ya miaka mitano inayoweza kuongezwa muda; Watanzania tu ndiyo wenye vigezo vya kupata aina hizi mbili za leseni. Ili kukidhi vigezo, mwombaji anatakiwa kumiliki ardhi ambayo itachimbwa madini ya dhahabu, kujua alama (coordinates) za eneo tarajiwa la kuchimba madini, na kuwasilisha nyaraka zinazohitajika kwa ajili ya maombi ya leseni. Mtaalamu wa madini kutoka idara ya madini ya mkoa atahakiki nyaraka za maombi kabla ya kutoa leseni. Gharama za maombi ya leseni kwa wachimbaji madini wadogo wadogo ni shillingi 50,000 kwa ajili ya ada ya usajili na shilingi 50,000 kwa ajili ya ada ya kuiandaa. Ada ya leseni ya uchimbaji madini ni shilingi 80,000 kwa hekta na mchimbaji anaweza kumiliki hekta 10. Mara tu leseni ikishatolewa, mmiliki anawajibika kisheria kwa shughuli zote zinazofanyika kwenye eneo lake, ikiwa ni pamoja na kufuata kanuni za uchimbaji madini, mazingira na usalama. Kanuni za uchimbaji madini zinazuia wamiliki wa leseni kuwahusisha watoto na vijana walio chini ya umri wa miaka 18 katika maeneo yao ya uchimbaji madini.

Idara ya madini ya mkoa pia ina jukumu la kuzuia shughuli zote za uchimbaji madini na biashara haramu katika mkoa huo, kukabiliana na athari za kimazingira, kusaidia wachimbaji wadogo kufanya shughuli zao kwa utaratibu mzuri zaidi, kuwapa msaada wa kitaalam,wachimbaji wadogo wadogo na kuboresha shughuli za uchimbaji madini mdogo mdogo.

Kwa mujibu wa maafisa madini wa mkoa, kuna wachimbaji wadogo wadogo 1,000 -2000 waliosajiliwa katika mkoa wa Geita (ambapo wilaya ya Bukombe inapatikana) na 800 katika mkoa wa Mbeya (ambapo wilaya ya Chunya inapatikana) wakati wa utafiti wilaya ya Songwe bado ilikuwa chini ya ofisi ya madini ya mkoa wa Mbeya). Wachimbaji waliosajiliwa wanapata msaada wa kitaalamu na wa aina nyingine, wakati wowote wanapohitaji, kutoka kwenye idara ili kuboresha shughuli zao za uchimbaji madini. Wachimbaji wadogo wadogo waliopewa leseni pia wana chama chao kinachojulikana kama GEREMA (Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Geita) na MBEREMA (Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Mbeya).

1.1.2. Uchimbaji usio rasmi/usio halali

Wachimbaji madini wadogo wadogo wasio rasmi wanaonekana kama wanaendeleza matatizo katika migodi na kwa kiasi kikubwa kukiuka sheria na kanuni za uchimbaji madini. Hii inaweza kuwa kwa sababu hawana ujuzi wa kutosha, kwa kuwa hawakupata mafunzo juu ya uchakataji madini wala madhara yake. Mara nyingi, wachimbaji wasio rasmi hufanya shughuli katika migodi isiyo na leseni na asili ya shughuli zao huwa ni za muda mfupi tu na uvamizi wa machimbo ya dhahabu. Kwa kuwa ni wachimbaji wadogo, shughuli zao hazina udhibiti wowote na husababisha mazoea ya uchimbaji hatari na uharibifu mkubwa wa mazingira, mbaya zaidi husababisha ongezeko la uchafuzi wa zebaki na ukataji mkubwa wa misitu. Hawana chama cha uchimbaji madini na hawastahili kuwa wanachama wa GEREMA/MBEREMA kwa sababu ya masharti ya kumiliki leseni ya madini. Watoto na wanawake wengi wameajiriwa katika hii migodi midogomidogo isiyo rasmi.

1.2. Watoto walioko kwenye machimbo ya madini

Shirika la Kazi Duniani (ILO) linachukulia kuwa uchimbaji madini ni mojawapo ya aina mbaya zaidi ya ajira za watoto (WFCL) kwa sababu ya hatari za kiafya na ustawi kutokana na kazi yenyewe. Wachimbaji wa umri wowote hawana ujuzi, hutumia kidogo au hawatumii kabisa mavazi ya kuwakinga wasipate madhara na huchimba madini kwa mikono yao mitupu au kwa kutumia zana duni. Afya zao ziko hatarini kwa sababu kuna uwezekano wa kuathiriwa na vumbi au madini mengine, vitu vinavyolipuka, zebaki, sianidi (cyanide), na kemikali zingine. Wako katika hatari ya kupata ajali na kuangukiwa na kifusi na mara nyingi hubeba mizigo mizito. Uchafuzi wa mazingira, chakula, na maji na usafi wa mazingira duni huongeza hatari ya ugonjwa ndani ya jamii katika maeneo ya machimbo ya madini. Matumizi ya madawa ya kulevya na pombe ni ya kawaida katika makambi ya wachimbaji madini na yanaweza kuathiri jamii zinazozunguka. Kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini kwa kiasi kikubwa hujumuisha makazi yasiyo ya kudumu bila familia zao, wahamiaji wa kiume wenye kipato cha kutosha, na kuchangia kwa kiasi kikubwa vitendo vya unyanyasaji wa kingono kwa watoto na watu wazima wanaofanya biashara ya ngono, na hatari zinazohusiana na afya na kijamii.

Mazingira mabaya ya kufanyia kazi ambapo kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo wa madini hufanyika yana athari mbaya hususan kwa watoto wanaofanya kazi katika migodi. Kama Shirika la

Kazi Duniani (ILO) linavyoelezea, watoto wanakabiliwa na "hatari kama vile watu wazima-kufunikwa na kifusi, kuangukiwa na mawe/miamba, sumu ya zebaki, kukosa hewa ya oksijeni-lakini, kwa sababu miili yao na uwezo wa kufanya maamuzi bado vinaendelea kukua, kuna uwezekano wa kupata majeraha zaidi ... na [watoto] wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuathiriwa na mtindo wa maisha yasiyokuwa na udhibiti kwenye makambi ya machimbo ya madini. Wale ambao hawafanyi kazi moja kwa moja katika mashimo hutoa huduma kwa wale wanaofanya. Idadi kubwa ya watoto katika maeneo ya machimbo ya madini tayari wamejiingiza kwenye ukahaba. Karibia wote hakuna anayepata elimu nzuri." [4]

Uwezekano wa kuathiriwa na zebaki mara nyingi huwa ni mkubwa kwa watoto, kutokana na uzito wa miili yao kuwa mdogo na tabia za utoto ambazo zinaongeza uwezekano mkubwa wa kuweza kuathiriwa (k.m., kuweka mikono yao midomoni baada ya kugusa mchanga au udongo moja kwa moja).[5] Watoto wanaojihusisha na kazi za mikono na uchimbaji mdogomdogo waliohojiwa kwa ajili ya ripoti ya mwaka 2013 ya shirika la Haki za Binadamu Duniani katika wilaya ya Chunya (Mkoa wa Mbeya), Kahama na Shinyanga (mkoa wa Shinyanga) waliteseka kutokana na uchovu, maumivu ya kichwa, maumivu ya misuli, malengelenge, na uvimbe. Utafiti unaonesha kuwa matatizo ya muda mrefu yanaweza kujumuisha magonjwa ya kupumua, matatizo ya misuli na mifupa, na sumu ya zebaki. [6]

Mipango ya sasa ya Pact nchini Kolombia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo [inayolenga dhahabu, bati, tantalum, madini ya kutengeneza chuma cha pua (tungsten), na makaa ya mawe] imesisitiza haja ya kuorodhesha watoto ili kujua ni "aina gani" ya watoto waliopo (kwa mfano, watoto wanaofanya kazi kwa maslahi yao, watoto wanaofanya kazi katika vitengo vya familia, vijana wanaojihusisha na uchimbaji wa madini baada ya kutoka shule, na/au vijana wenye watoto wao) kuamua vipaumbele na ufanisi wa majibu.

1.3. Mfumo wa taifa wa kisheria

Tanzania imeridhia mikataba kadhaa ya kimataifa inayohusu ajira za watoto. Mikataba hii ni pamoja na Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto (UN CRC); Itifaki ya hiari ya Umoja wa Mataifa juu ya Migogoro ya Kivita; UN CRC Itifaki ya hiari ya Umoja wa Mataifa juu ya Uuzaji wa Watoto, Biashara ya ngono kwa Watoto na Ponografia; Itifaki ya Palermo juu ya Usafirishaji wa Watu, hususan wanawake na watoto; Mkataba wa ILO Namba 138 wa mwaka 1973 juu ya umri mdogo wa kuajiriwa na kufanya kazi; na Mkataba wa ILO Namba 182 wa mwaka 1999 juu ya Aina mbaya zaidi ya Ajira za watoto. Sheria ya Watoto Tanzania, Sheria ya Mahusiano Kazini na Ajira, na Kanuni za Uchimbaji madini, zinakataza watoto chini ya miaka 18 kujihusisha na kazi za hatari ikiwa ni pamoja na uchimbaji madini. Kwa hiyo, chini ya sheria za kimataifa na za ndani, serikali ya Tanzania inalazimika kulinda watoto dhidi ya ukiukwaji wa haki zao, ikiwa ni pamoja na Aina Mbaya Zaidi ya Ajira za watoto (WFCL) kama vile uchimbaji madini na biashara ya ngono.

1.4. Mwitiko wa kitaifa

Ingawa idadi kadhaa ya sera na programu za kutokomeza ajira za watoto zimetekelezwa[7] na licha ya kuwa kinyume cha sheria, mwitiko mdogo wa serikali na mambo ya kiutamaduni na kijamii[8] yanachochea watoto kujihusisha na uchimbaji madini. Utafiti wa Kitaifa wa Ajira za watoto wa mwaka 2014 ulionesha kuwa karibia watoto 31,000 wanajihusisha na uchimbaji madini na mawe kwa wastani wa saa 20 kwa wiki, idadi ya wasichana ikiwa ni ndogo zaidi kuliko wavulana. Nusu ya watoto wote katika utafiti huu ambao walihusika katika kazi ya aina yoyote ya hatari (siyo uchimbaji madini tu) waliripotiwa kuwa na majeraha, ugonjwa, au afya duni, na asilimia 20 waliripotiwa kufanya vibaya shuleni. Ingawa wazazi wengi waliohojiwa kama sehemu ya Tathmini ya Haki za Binadamu[7] walisema kuwa hawakuwatuma watoto wao kwenda kwenye migodi na watoto wengi hawakutaka kufanya kazi huko, umaskini, usimamizi duni wa maofisa kazi, kutotambua athari za kemikali za hatari kiafya, utekelezaji duni wa sera za elimu, na msaada hafifu, hususan kwa yatima, kuenea uchimbaji madini kwa watoto katika jamii nzima na kuwa vigumu kuzuia.

1.5. Mradi wa USAID Kizazi Kipya

Pact, pamoja na wadau wake, watatekeleza mpango mpana wa kuboresha huduma za afya na kijamii kwa watoto walioko kwenye machimbo ya madini (CIM). Muundo wa programu hiyo unafafanuliwa na matokeo ya utafiti na lengo la ripoti hii.

Mpango huu wa Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini ni sehemu ya mradi mkubwa zaidi wa USAID Kizazi Kipya (2016-2021), ambao una lengo la kufikia watoto yatima milioni 1 na watoto walioko kwenye mazingira hatarishi (OVC) katika kaya 350,000 nchini Tanzania, na kuimarisha uchumi, huduma za afya na kijamii. Washirika wote na majukumu yao kwa kuanza na Pact ni (uimarishaji wa kiuchumi na usimamizi wa washirika wote), Aga Khan Foundation (elimu na maendeleo ya awali ya watoto), Restless Development (vijana), Elizabeth Glaser Pediatric AIDS Foundation (utoaji wa huduma za kliniki kwa watoto wenye maambukizi ya VVU), Railway Children of Africa (watoto wanaoishi/wanofanya kazi mitaani), na Taasisi ya Afya Ifakara (watoto kwenye utafiti wa uchimbaji madini).[2]

[6] Human Rights Watch. 2013. *Toxic Toil: Child Labor and Mercury Exposure*. http://www.hrw.org/reports/2013/08/28/toxic-toil-0

[7] International Labor Office, Fundamental Principles and Rights at Work (FUNDAMENTALS), and Tanzania National Bureau of Statistics. 2016. *Tanzania national child labor survey 2014: Analytical Report*. Geneva: ILO.

[8] Human Rights Watch 2013.

1.6. Malengo ya utafiti

Kipengele cha tathmini ya utafiti kililenga kushughulikia malengo makuu mawili ya utafiti.

1. Kutathmini njia za ushiriki wa watoto katika shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini na tabia zinazojenga mazingira katika jamii. Malengo maalum yalikuwa ni:

i. Kutambua wadau muhimu na huduma zinazopatikana kwenye maeneo ya utafiti
ii. Kujua mitazamo na mienendo iliyopo kuhusu ajira za watoto walioko kwenye machimbo ya madini na mahusiano ya mamlaka
iii. Kujua sababu, mazingira, na tabia za watoto wanaojihusisha na uchimbaji madini
iv. Kujua hatari na faida zinazohusiana na uchimbaji madini kwa watoto na vijana
v. Kuelewa mahitaji muhimu ya huduma za watoto katika machimbo ya madini na jamii zao

2. Kutumia matokeo ya utafiti kwenye lengo 1 kuelezea muundo sahihi na halisi wa utekelezaji kwa ajili ya utoaji wa huduma za afya na kijamii zilizoboreshwa kwa watoto walioko kwenye machimbo ya madini. Malengo maalum yalikuwa:

i. Kujadili matokeo ya utafiti na washirika wote wa mradi wa USAID Kizazi Kipya na wadau wengine, ikiwa ni pamoja na wawakilishi kutoka kwenye wilaya na kata za utafiti, Wizara ya Afya, Idara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee na Ustawi wa Watoto na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kuandaa mapendekezo kwa ajili ya utekelezaji
ii. Kufanya mikutano ya kutoa mrejesho na jamii kwa ajili ya kupanga rasilimali zilizopo katika jamii na kutambua mahitaji ya kuimarisha uchumi wa kaya za wazazi na walezi wa Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini ili kuelezea uandaaji wa mpango wa utekelezaji.

2. Mbinu ya Utafiti

2.1. Maeneo ya utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika wilaya za Bukombe, Chunya, na Songwe. Katika kila wilaya, shughuli za utafiti zilijikita kwenye kata moja iliyochaguliwa kwa makusudi: Igulwa (Bukombe), Matundasi (Chunya), na Saza (Songwe). Uchaguzi wa kata ulifanyika baada ya majadiliano na watendaji wa wilaya na ziara za utambuzi wa maeneo ya utafiti zilizofanywa awali na watafiti wakuu kabla ya tathmini hii kufanyika. Wilaya ambazo utafiti unaweza kufanyika zilitambuliwa kabla na Kizazi Kipya. Uchaguzi wa mwisho ulizingatia uwepo wa shughuli za uchimbaji mdogomdogo wa madini zinazoendelea na kutokuwepo kwa mradi wowote hususan unaolenga kuwasaidia Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini.

2.2. Muundo wa Utafiti

Tathmini hii ilitumia mtindo wa uchunguzi wa kifani (case study design) kwa kutumia njia mbalimbali za ukusanyaji taarifa, hususan mahojiano ya watu muhimu (KIIs), majadiliano ya vikundi (FGDs), na mahojiano ya kina (IDIs). Muundo huu ulihakikisha uwakilishi wa mawazo, maoni, uzoefu na mapendekezo ya wadau mbalimbali wa Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini katika maeneo husika ya utafiti. Kupata maoni mengi kwenye baadhi ya maswali yaleyale kumewezesha kupima maoni kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya taarifa. Jedwali la 1 linaonesha makundi ya washiriki kulingana njia ya ukusanyaji taarifa na idadi ya majadiliano/mahojiano kwa kila wilaya na kila njia.

Jedwali 1: Aina ya washiriki, mbinu za mahojiano na idadi ya mahojiano kwa kila eneo la utafiti

Washiriki na njia za ukusanyaji taarifa	Idadi ya majadiliano kwa kila eneo la utafiti			Jumla ya majadiliano
	Bukombe	Chunya	Songwe	
Mahojiano ya kina				
Wachimbaji watoto	6	5	4	15
Watoto ambao hawako kwenye migodi	6	5	4	15
Wazazi wachimbaji	5	2	2	9
Wamiliki wa migodi	5	2	2	9
Vituo vya kutolea huduma za afya	2	1	2	5
Asasi za kiraia (AZAKI)	4	0	0	4
Viongozi wa kijamii	4	2	2	8
Watendaji/maofisa wa wilaya	2	2	1	5
Walimu wa shule	2	1	1	4
Mahojiano ya watu muhimu				
Watu wenye ushawishi	2	1	2	6
Majadiliano ya kikundi				
Wanaume	2	1	1	4
Wanawake	2	1	1	4
Jumla ya idadi kwa kila eneo	**42**	**23**	**22**	**88**

2.2.1. Majadiliano ya kikundi na wanajamii wa kawaida

Majadiliano ya kikundi nane na wanajamii wa kawaida yalifanyika. Ili kuwezesha utoaji huru wa mawazo na maoni kuhusu masuala yanayojitokeza, majadiliano ya kikundi yalifanyika tofauti kwa wanaume na wanawake. Idadi ya washiriki katika kila kikundi ilikuwa kati ya 8-12, na kufanya jumla ya washiriki kuwa 84. Majadiliano haya yalilenga kutathmini kwa mapana zaidi mitazamo ya jumla ya jamii, maoni, na mienendo kuhusu ushiriki wa watoto katika shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini. Majadiliano ya Kikundi yalisaidia kupata taarifa nyingi kuhusu desturi, mawazo, na maoni ya jamii dhidi ya ajira za watoto na sababu za msingi za ajira za watoto katika maeneo husika. Pia, masuala ya mabadiliko ya uongozi kuhusiana na umri na wajibu wa kijinsia yaliulizwa.

Washiriki wa Majadiliano ya Kikundi walichaguliwa kwa makusudi kutoka kwa wanajamii wa jamii husika katika maeneo ya machimbo ya madini kwa msaada wa viongozi wa jamii. Vigezo vya kushiriki vilikuwa ni kuwa na uelewa na ufahamu wa maeneo ya machimbo ya madini na kuishi katika eneo husika kwa angalau miaka mitano. Watu hawa waliaminika kuwa na ufahamu wa kutosha sio kuhusu tu jamii na shughuli zinazofanywa, bali pia mazingira ya kutengeneza ajira za watoto katika migodi.

2.2.2. Mahojiano ya watu muhimu

Mahojiano ya Watu Muhimu sita (KII) yalifanyika na watu wenye ushawishi katika jamii ili kufahamu na kupanga shughuli mbalimbali, mashirika, na taasisi za maendeleo zilizopo katika maeneo ya utafiti na ambazo kazi zao zinahusiana na Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini na aina ya shughuli husika ambayo hufanyika. Washiriki wa Mahojiano ya Watu Muhimu (KII) walielezea ufahamu wao kuhusu asili ya ajira za watoto na huduma za kijamii zilizopo kwenye maeneo ya utafiti kulingana na nafasi zao, maarifa na uelewa wao. Mwongozo wa Mahojiano ya Watu Muhimu uliandaliwa kwa ajili ya mahojiano.

Washiriki wa Mahojiano ya Watu Muhimu (KII) walichaguliwa kwa makusudi kwa kushauriana na washiriki wa Majadiliano ya Kikundi (FGD), ambao walipendekeza watu wawili waliofikiri walikuwa na ushawishi mkubwa katika jamii na ambao waliamini walikuwa na uelewa mkubwa wa jamii, tabia yake, na shughuli zinazoendelea katika maeneo hayo. Majina yaliyopendekezwa yalipelekwa kwa viongozi wa kijiji ambao waliisaidia timu ya utafiti kuwapata hawa watu. Mahojiano ya Watu Muhimu mawili yalifanyika katika kila eneo la utafiti, na kufanya jumla ya mahojiano sita.

2.2.3. Mahojiano ya Kina

Kwa ujumla, Mahojiano ya Kina (IDI) 74 yalifanyika na watu mbalimbali ili kupata tarifa nyingi na za kina kuhusiana na mitazamo, mawazo, hisia, na uzoefu wa watu kuhusiana na ajira za watoto kwenye migodi. Mabadiliko ya Mahojiano ya Kina na mwitiko wao dhidi ya lugha na dhana ya mtu mmoja mmoja ilisaidia uelewa wa kina na udodosaji wa kina kuhusu uzoefu wa maisha wa mtu mmoja mmoja katika mazingira ya kijamii ya machimbo ya madini, asili ya ajira za watoto, mwelekeo wa maisha ya watoto na familia zao zilizojihusisha katika uchimbaji madini, na miundo ya ufanyaji maamuzi katika jamii za wachimbaji madini.

Mahojiano ya Kina yalifanyika kwa kuhoji mtu mmoja mmoja kutoka kwenye makundi yafuatayo, kama ilivyofafanuliwa kwenye Jedwali la 2.

Watoto wenye umri wa miaka 12-18 na elimu zao kuanzia ambaye hajasoma mpaka kidato cha III. Wachimbaji ambao sio watoto na vijana walikuwa ama bado wanasoma, walijiingiza katika biashara ndogo ndogo, au walibaki nyumbani.

Jedwali la 2: Mchanganuo wa wahojiwa wa mahojiano ya kina

Kundi la Mahojiano ya Kina	Idadi ya waliohojiwa	Lengo la kuhoji kundi hili
Watoto waliojiingiza katika shughuli za uchimbaji madini	15	Ili kupata uelewa wa kina wa watoto/vijana wenyewe kuhusu njia za kufanya kazi katika migodi, shughuli za uchimbaji madini zilizofanywa, uzoefu wao, na faida na hatari zinazohusiana na shughuli za uchimbaji madini kwa ujumla.
Watoto wasiofanya kazi kwenye migodi	15	
Waganga wafawidhi wa vituo vya kutolea huduma za afya vilivyo karibu ambavyo hutoa huduma kwenye jamii za wachimbaji	5	Ili kupata ufahamu wa kina kuhusu matatizo ya kawaida ya afya yaliyopo ambayo yanahusishwa na shughuli za uchimbaji madini katika jamii na uzoefu katika kukabiliana nayo, ikiwa ni pamoja na ajira za watoto, VVU, na mimba za utotoni.
Walimu wakuu wa shule zilizoko karibu na maeneo ya machimbo ya madini	4	Kupata ufahamu wa kina kuhusu mitazamo ya walimu wa shule kuhusu ajira za watoto katika migodi, mahusiano yake na mahudhurio ya watoto shuleni na jinsi ya kukabiliana na suala hilo
Wamiliki wa migodi/Wafadhili	9	Ili kupata uelewa wa kina wa tabia zinazosababisha ajira za watoto katika migodi, shughuli za uchimbaji madini zinazofanywa na watoto, njia ya ushiriki, mapatano kuhusu malipo ya wachimbaji
Wazazi wa wachimbaji	9	

watoto		watoto, na ufanyaji maamuzi kuhusu mapato ya watoto wachimbaji.
Viongozi wa kijamii	8	Kuondoa mitazamo ya mtu mmoja mmoja, maoni, na mienendo kuhusu ajira za watoto na tabia zake na kuhusu hatua za kukabiliana na hali hiyo
Maofisa/Watendaji wa Wilaya	5	
Wawakilishi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali	4	

Upataji washiriki wa mahojiano ya kina

Mbinu ya kupata washiriki kwa kurusha mpira na kuwachagua kwa makusudi zilitumika kuwapata washiriki wa mahojiano ya kina.

Kurusha mpira

Mbinu ya kupata washiriki kwa kurusha mpira ilitumika kuwapata watoto wanaofanya kazi katika migodi. Mawasiliano ya kwanza na mtoto/kijana ambaye anajihusisha na uchimbaji madini au shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini yalifanyika kwa msaada wa viongozi wa jamii. Mtoto/kijana huyu alitambulishwa kwa timu ya utafiti na timu ilimwelezea mtoto/kijana kuhusu utafiti na shughuli zake zinazohusiana. Mahojiano yalianza tu baada ya kufahamiana na kupata ridhaa.

Baada ya mahojiano, mtoto aliombwa kuitambulisha timu ya utafiti kwa mmoja wa marafiki zake ambaye pia anajihusisha na kazi zinazohusiana na uchimbaji wa madini. Mchimbaji mtoto/kijana alipomtambulisha mwenzake kwa timu ya utafiti, utaratibu ulikuwa ni uleule wa kumwelezea mchimbaji mtoto kuhusu utafiti na shughuli zinazohusiana na utafiti na kwa ajili ya kuomba ridhaa yake ya kushiriki katika utafiti na kuiunganisha timu ya utafiti kwa marafiki zake wengine. Utaratibu wa kuwapata uliendelea mpaka idadi ya wachimbaji watoto ilipotimia, au kabla ya kutimia kama taarifa zinazohitajika zilipatikana.

Uwezo wa kupata washiriki kwa njia ya kurusha mpira (snowball) kwa kutumia mtandao wa kijamii na mahusiano ya kiuaminifu ya watoto waliotambuliwa ulihakikisha upatikananji wa wachimbaji watoto kwa ajili ya utafiti. Watoto wale tu ambao walikuwa wamejiingiza katika shughuli za uchimbaji wa madini kwa kipindi cha angalau miezi sita wakati huo huo wa utafiti walikuwa wanastahili kujumuishwa ili kuhakikisha kwamba walikuwa wamejihusisha kwa muda wa kutosha na kupata uzoefu kuhusu masuala ya uchimbaji madini. Ili kuepuka kuwashirikisha watoto kutoka kwenye mtandao mmoja wa kijamii, vikundi mbalimbali vya watoto vilifikiwa wakati wa mchakato wa kuwapata.

Kuwapata washirki kwa njia ya makusudi

Njia ya kupata washiriki kwa makusudi kwa ajili ya Mahojiano ya Kina ilitumika kwa msaada wa viongozi wa kijiji ili kuwapata:

- Watoto katika jamii ambao hawajihusishi na shughuli zinazohusiana na uchimbaji wa madini
- Wawakilishi wa AZAKi/taasisi zinazotekeleza programu za kuwasaidia Watoto Yatima na Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi na wenye VVU na kundi la wachimbaji
- Wazazi/walezi wachimbaji wa watoto katika jamii za wachimbaji madini
- Watoa huduma za afya kutoka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya katika jamii za wachimbaji madini
- Wafadhili wa migodi/wamiliki wa maeneo ya machimbo ya madini
- Viongozi wa jamii ambao walichaguliwa kwa nafasi zao katika jamii, ikiwa ni pamoja na watendaji wa kijiji na kata, wahudumu wa afya ya jamii, na waratibu wa elimu wa kata

2.3. Ukusanyaji taarifa na uchambuzi

2.3.1. Miongozo ya ukusanyaji taarifa za majaribio

Miongozo ya ukusanyaji taarifa za utafiti wa majaribio na shughuli za ukusanyaji wa taarifa kwa ujumla zilifanywa na timu ya watafiti watano wenye uzoefu na sifa bora mwezi Mei 2017. Kabla ya utafiti wa majaribio, washiriki wa timu ya utafiti walipatiwa mafunzo na mtafiti mwandamizi kuhusu mradi ili kuhakikisha wanaelewa kwa kina malengo ya mradi na mahitaji ya matokeo kwa ajili ya

uthabiti na ukamilifu. Washiriki wa timu ya utafiti walikuwa tayari wamepata mafunzo mbalimbali kama hayo katika siku za nyuma kwenye kazi zingine katika taasisi na mashirika mbalimbali. Hata hivyo, walipatiwa tena mafunzo kuhusu mambo yaliyohusiana na ufanyaji Mahojiano ya Kina (IDI), Majadiliano ya Kikundi (FDGs), na Mahojiano ya Mtu Muhimu (KII), ikiwa ni pamoja na kuwa wasikilizaji wazuri, wachukua kumbukumbu, matumizi ya vinasa sauti, mbinu za kudodosa, na kunakili kwa usahihi kutoka kwenye sauti kwenda kwenye maandishi. Baada ya mafunzo, timu ya utafiti iliifanyia majaribio miongozo ya ukusanyaji taarifa katika kata ya Katente, kata hii ni tofauti na zile kata tatu zinazohusika katika shughuli za ukusanyaji taarifa halisi. Utafiti wa majaribio ulisababisha kufanyika mabadiliko madogo tu yanayohusiana na lugha iliyotumika, na sio mabadiliko ya maudhui ya madodoso. Kwa hiyo, wakati wa uchambuzi, tulijumuisha matokeo ya utafiti wa majaribio.

2.3.2. Ukusanyaji taarifa halisi/rasmi

Mahojiano yote yalifanyika kati ya mwezi Mei na Julai 2017. Mahojiano ya Kina (IDI) na mahojiano ya Watu Muhimu (KIIs) yalifanyika kama mahojiano ya ana kwa ana, wakati Majadiliano ya Kikundi (FGDs) yalifanyika kwa kumhusisha mwezeshaji wa majadiliano na mchukua kumbukumbu. Mahojiano haya na majadiliano yalifanyika katika mazingira ambayo yaliruhusu faragha ya kutosha na washiriki walijisikia huru kutoa maoni yao. Shughuli zote za ukusanyaji taarifa zilifanyika kwa lugha ya Kiswahili, lugha inayozungumzwa na washiriki wote wa utafiti. Ili kupata taarifa za kina, mahojiano yote na majadiliano ya vikundi yalirekodiwa sauti baada ya kupata idhini ya mdomo kutoka kwa washiriki wa utafiti. Aidha, maelezo ya kina yalichukuliwa wakati wa mahojiano na majadiliano ili kuongeza taarifa za ziada kwenye rekodi za sauti. Ili kulinda utambulisho wao, washiriki wa utafiti waliombwa kutumia majina ya bandia, sio majina yao halisi. Sauti zilizorekodiwa zilinakiliwa kama zilivyo kwa njia ya maandishi ya kieletroniki ndani ya saa 48 baada ya kurekodiwa. Hii iliruhusu kufuatilia kwa urahisi na ufafanuzi wa masuala yaliyojitokeza wakati wa shughuli za ukusanyaji taarifa. Nyaraka za Kiswahili zilihakikiwa kwa kusikiliza sauti ili kuangalia ubora na kiongozi wa timu ya ukusanyaji taarifa kabla ya kuanza uchambuzi wa taarifa hizo.

2.3.3. Uchambuzi wa taarifa na uthibitishaji

Uchambuzi wa taarifa ulikuwa ni mchakato endelevu kwa kuanzisha mada za majaribio na mada ndogo wakati na baada ya ukusanyaji taarifa. Taarifa ziliingizwa kulingana na mada ndogo na hatimaye zilijumuishwa kwenye mada kuu. Uchambuzi huu wa mada ulifanyika kwa kutambua, kuchambua, na kutoa ripoti kwa mpangilio (mada) ndani ya taarifa hizo. Utaratibu huu ulifanyika kwa kupima nadharia zilizopo na kubuni nadharia mpya kwa kutumia nakala za Kiswahili. Nukuu zilizotumika katika ripoti hii tu ndizo zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiingereza. Uchambuzi ulifanywa na wanasayansi waandamizi wawili wa kijamii ambao walikuwa sehemu ya timu ya ukusanyaji taarifa na ambao walifikia makubaliano kuhusu maana ya nukuu hizo.

Kisha, kama mkakati wa uthibitishaji, matokeo ya uchambuzi yalirejeshwa kwa wazazi/walezi katika jamii za wachimbaji madini na kwa wajumbe wa kamati ya maendeleo ya kata. Hii ilifanyika katika mikutano miwili tofauti katika kila wilaya, mnamo Septemba 2017. Jumla ya watu 48 walihudhuria mikutano ya wazazi (Chunya, 15; Bukombe, 18; na Songwe, 15).

Wajumbe wa kamati ya kata waliojumuishwa ni pamoja na wenyeviti wote wa vijiji/vitongoji na wataalamu wanaofanya kazi katika kata, kama vile maafisa watendaji wa kata, maafisa elimu wa kata, maafisa ugani wa kata, watendaji wa kijiji, viongozi wa baraza, katibu tarafa, viongozi wa dini, na maafisa mipango na maendeleo ya jamii kutoka kwenye wilaya husika. Washiriki arobaini na tisa walishiriki katika mikutano ya mrejesho ya kamati ya kata (Chunya, 16; Bukombe, 18; na Songwe, 15).

Utaratibu ulianza kwa timu ya utafiti kuwasilisha matokeo kuhusu mada maalum. Washiriki waliombwa kuchangia na kutoa mitazamo, uelewa, na maoni yao kwa kila ujumbe uliowasilishwa. Washiriki pia walipewa fursa ya kurekebisha na kuthibitisha matokeo muhimu yaliyowasilishwa. Matokeo yote ya utafiti yaliyowasilishwa yalithibitishwa kwenye mikutano na masuala mapya machache yalijitokeza, yakionesha kwamba ukusanyaji taarifa wa awali ulikuwa kamilifu na sahihi. Masuala mapya yaliyojitokeza yamejumuishwa kwenye Sehemu ya 3.

2.4. Masuala ya kimaadili

Utafiti huu ulipewa idihini ya kimaadili na Bodi ya Uhakiki wa Kitaasisi ya Taasisi ya Afya Ifakara na Kamati ya Taifa ya Kuratibu Utafiti wa Kimatibabu nchini Tanzania iliyo chini ya Taasisi ya Taifa Kwa ajili ya utafiti wa kimatibabu. Kibali cha kufanya utafiti katika maeneo ya utafiti kiliombwa kutoka kwa mamlaka za wilaya na kutoka kwa maafisa watendaji wa kata na vijiji katika maeneo husika ya utafiti.

Ridhaa ya kimaandishi ilipatikana kama ifuatavyo: Mchakato wa taarifa ulielezea haki ya wahojiwa watakaoshiriki kukubali au kukataa kuhojiwa, haki ya kusitisha mahojiano wakati wowote, makadirio ya urefu wa mahojiano, masharti yasiyo ya malipo ya ushiriki, na usiri wa taarifa iliyotolewa na mhojiwa. Ridhaa ya kimaandishi ya kushiriki katika utafiti ilipatikana kutoka kwa washiriki wote wa utafiti. Katika hali zote, ikiwa mhojiwa hakujua kusoma na kuandika, aliweka dole gumba mbele ya shahidi yake, ambaye pia alisaini kwa ajili ya uthibitisho wa mchakato wa ridhaa.

Ridhaa kwa washiriki watoto au vijana wenye miaka chini ya kumi na nane iliombwa kupitia wazazi wao au walezi. Kama mzazi au mlezi anayetambuliwa kisheria hakuwepo, afisa wa serikali au viongozi wa jamii katika eneo la utafiti ambapo mtoto anaishi aliombwa kutoa ridhaa kwa niaba ya wazazi/walezi. Mbali na idhini ya wazazi/walezi, watoto na vijana wadogo wenyewe waliombwa kutoa ridhaa kwa maandishi.

Taarifa zote na rekodi za sauti zilitambulishwa kwa utambulisho wa pekee ambao haukuweka wazi majina yao na hakuna mahojiano wala majadiliano yoyote yaliyounganishwa na wahojiwa husika.

3. Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inatoa mjumuisho wa matokeo ya utafiti. Nukuu kutoka kwa wadau/wahojiwa wa utafiti kuhusu mawazo/matokeo yaliyojadiliwa yameandikwa kwenye visanduku vyenye maandishi yenye rangi ili kuelezea sauti za washiriki.

3.1. Wadau

Utafiti huu ulihusisha wadau kadhaa katika jamii ambao wanahusika moja kwa moja au siyo moja kwa moja katika kufanya shughuli zinazohusiana na uchimbaji wa madini. Wadau hao ni pamoja na:

- Wamiliki wachimbaji: Watu ambao wanamiliki mashimo ya migodi, mashine za kusaga mawe, na maeneo ya kuoshea madini na watu wanaokusanya masalia ya udongo baada ya mchanga kuchenjuliwa ili kupata dhahabu kwa kutumia zebaki
- Vikundi vya wachimbaji ambao hujumuika pamoja ili kufanya shughuli za uchimbaji madini, kwa mfano kikundi cha Washirika huko Bukombe
- Mama Lishe: Wale wanomiliki vibanda vya chakula, wapishi, na kupeleka chakula kwa ajili ya kuuza kwa wachimbaji kwenye maeneo ya machimbo ya madini
- Wamiliki wa baa: Watu wote wanaoendesha biashara ya baa na migahawa
- Wachimbaji watoto: Watoto wanaofanya kazi ama moja kwa moja za uchimbaji madini au kutoa huduma ili kusaidia shughuli za uchimbaji wa madini
- Wanajamii wa kawaida katika maeneo ya migodi: Inaonekana katika utafiti kwamba mwanajamii yeyote anaweza kuwa mwajiri wa watoto maadam ana (mzigo), mawe ya kuchakatwa ili kupata dhahabu.

3.2. Mtoto ni nani kwa mujibu wa jamii

Mawazo, maoni, mitazamo, na mienendo kuhusu nani anayeonekana kuwa mtoto katika jamii ilidodoswa wakati wa Majadiliano ya Kikundi (FGDs). Katika kutoa maoni yao, mara kwa mara washiriki walirejea kanuni za serikali ya Tanzania au sheria ambazo zinafafanua kuwa mtoto ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka 0 hadi 18. Hata hivyo, wao pia walisema kuwa umri wa mtu sio kigezo pekee kinachotumiwa kumchukulia mtu kuwa ni mtoto katika jamii. Kwa kufafanua hili, mawazo mbalimbali na maoni yalitolewa. Wengi walisema kwamba mtoto ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka 0 mpaka atakapomaliza shule. Wengine walisema kuwa mtoto anatambuliwa kwa tabia yake (tabia za kitoto) na/au anapokuwa tegemezi kwa wazazi wake au walezi kwa mahitaji yote ya msingi na maisha. Tofauti na wavulana, ilielezwa kuwa msichana anachukuliwa kuwa ni mtoto anapokuwa na umri wa miaka 0 hadi 13 kwa sababu wasichana wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuanza kuzaa wakiwa na miaka 14. Kwa ujumla, katika maeneo ya utafiti, watu wenye umri wa miaka 15-18 ambao hawaangukii kwenye sifa zilizotajwa hapo juu hawachukuliwi kama ni watoto; wanachukuliwa kama watu wazima na wanaruhusiwa kutekeleza wajibu na majukumu ya watu wazima. Aidha, kuwa mwanafunzi ni sifa muhimu ya kumchukulia mtu kuwa ni mtoto, wakati kuhitimu masomo ni ishara ya kuingia katika ukomavu, hivyo hawezi kuchukuliwa ni kama mtoto tena.

Tafsiri ya serikali, kwamba mtu yeyote mwenye chini ya miaka 18 ni mtoto, haiwezekani kutumika katika mazingira haya, katika mazingira yetu mtu anachukuliwa kuwa ni mtoto ikiwa kama anasoma au la.
- Majadiliano ya Kikundi, (FGD) Wanaume, Songwe

Katika jamii hii, mtu anachukuliwa kuwa ni mtoto anapokuwa na umri wa miaka 0 hadi 13, inamaanisha mtu ambaye bado hawezi kujitegemea, zaidi ya hapo anahesabiwa kuwa ni mtu mzima kwa sababu yeye tayari ameshaanza kujiingiza katika shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi kama vile uchimbaji wa madini na mambo mengine kuhusiana na mazingira haya.
- Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanawake, Bukombe

Sheria inasema mtoto ni mtu yeyote mwenye umri wa miaka 0 hadi miaka 18, lakini sasa hivi tunashindwa kusema hili kwa kweli ... katika mazingira yetu hapa unamkuta msichana mwenye umri wa miaka 14 ameshaolewa, jambo lile lile unaloliona kwa msichana mwenye umri wa miaka 18, kwa hiyo tunashindwa kuelewa, ndiyo maana tunasema akishafikisha umri wa miaka 14 tayari ni mtu mzima. - Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanaume, Chunya

Kwa Itumbi, ni sawa kusema watoto ni wale wenye umri wa miaka 14 lakini pia unakuta watoto wa rika hilohilo la miaka 14 tayari wanatekeleza majukumu ya watu wazima kama vile uchimbaji wa madini.
– Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanawake, Chunya

Kwa sababu katika umri wa miaka 14 wengi tayari wana watoto wao hivyo huwezi kumwita mtu mwenye mtoto na yeye mtoto. - Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanaume, Bukombe

3.3. Haki na majukumu yanayojulikana ya watoto

Washiriki wa utafiti walikuwa na uelewa wa pamoja wa shughuli zinazofaa kwa mtoto na anazopaswa kufanya. Iliongelewa kwenye Majadiliano ya Kikundi (FGD) kwamba watoto wanatakiwa kuhudhuria shule na baada ya hapo kuwasaidia wazazi wao kwa kufanya kazi za nyumbani. Maoni hayo hayo yalitolewa na viongozi wa jamii walioshiriki kwenye Mahojiano ya Kina (IDI), ambao walisema kwamba elimu ni jukumu la msingi la mtoto kwa sababu wanaamini kuwa shule inaweza kuboresha maisha ya baadaye ya watoto. Aidha, walisema, baada ya muda wa masomo shuleni na siku za mwisho wa juma, watoto wanatakiwa kuwasaidia wazazi wao kufanya shughuli za nyumbani, kama vile kuosha vyombo, kufanya usafi, kufagia, kufua nguo, kuwahudumia wadogo zao, kuchota maji, na kupika. Wakati elimu ilionekana kama shughuli ya msingi inayofaa mtoto kuifanya na kuchangia maendeleo ya akili ya mtoto, ushirikishwaji wa vijana katika kuwasaidia wazazi wao shughuli za nyumbani ulionekana kama njia ya kuwaandaa kuwa watu wazima wanaowajibika.

Ni haki ya mtoto kuhudhuria shule kwa sababu elimu ni urithi wake pekee.
- Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanawake, Bukombe
Wanahitaji kuwa shule ili kupata ujuzi wa kuendeleza akili zao, wanahitaji kukua kiakili.
- Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanaume, Songwe
Wakirudi kutoka shule wanapaswa kuwasaidia wazazi wao shughuli za kawaida za kaya kama vile kuosha vyombo, kufua nguo, kufagia, kupika, na kuwahudumia wadogo zao pamoja na shughuli nyingine ndogondogo nyumbani
- Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanawake, Chunya

Uhitaji wa watoto kuhudhuria shule pia ulioneshwa na watoto wenyewe, hususan wale ambao bado wako shuleni, wanasema kuwa kwenda shule na kuwasaidia wazazi kazi ndogondogo ni shughuli wanazostahili kuzifanya.

Mtoto anahitaji elimu na muda wa kujisomea, wanahitaji kuwasaidia wazazi wao kazi ndogondogo na si kazi ngumu kwenye migodi, uchimbaji wa madini ni kazi ngumu sana.
- Msichana mdogo asiyefanya kazi migodini, miaka 14, Songwe

Kipaumbele cha kwanza ni kusoma kwa sababu hakumdhuru mtoto badala yake kunamuandaa mtu kuwa na uelewa mzuri wa maisha yake ya baadaye. Pia nadhani ni sawa kuwasaidia wazazi shughuli ndogo ndogo nyumbani kwa sababu shughuli hizo hazisumbui ubongo na hazichoshi.

Ilitajwa kuwa wazazi wana wajibu wa kuhakikisha kuwa watoto wao wanapata malezi bora na upendo.

Ni jukumu la wazazi kuwatunza watoto wao na sio kuwaacha kufanya kazi, ni watoto bado wanahitaji upendo na malezi.

3.4. Mitazamo ya jamii kuhusu ajira za watoto

Ajira za watoto katika utafiti huu zilichukuliwa na watu wengi kama ushirikishaji wowote wa mtoto mwenye umri wa kwenda shule katika shughuli zenye lengo la kujipatia kipato

Ni pale unapomkuta mtoto badala ya kwenda shule yeye/anajihusisha na shughuli za uchimbaji madini kwa lengo ya kupata fedha iwe kwa uamuzi wake au wa wazazi wake.
- Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanawake, Bukombe

Baadhi ya washiriki walisema ajira za watoto ni ushirikishwaji wowote wa watoto katika kufanya shughuli ambazo zitawaondoa shuleni.

Kuwashirikisha watoto katika shughuli ambazo zitawaondoa shuleni au katika shughuli za kuingiza kipato kabla ya kufikia umri wa utu wazima.

- Watu wa Majadilliano ya Kikundi (FGD), Songwe

Washiriki walisema kwamba watoto wanashirikishwa katika shughuli mbalimabali ambazo kwa namna moja au nyingine zinaathiri masomo yao: kuchunga wanyama (Bukombe), kilimo (Chunya), uvuvi (Songwe), na shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini. Shughuli ya mwisho ilisemwa kuwa ni ya kawaida katika maeneo yote.

Ulikuwa ni mtazamo wa kawaida uliolezewa katika majadiliano ya kikundi kuwa si sahihi kuwashirikisha watoto katika shughuli ambazo zinawanyima haki yao ya kusoma. Kushirikisha watoto shughuli ngumu na za muda mrefu, kama vile zinazohusiana na uchimbaji madini, pia zimelaaniwa. Hii ni kwa sababu watoto wanaonekana kuwa bado hawajakomaa na viungo vyao ni vilaini, kwa hiyo wanaweza kuumia kwa urahisi

Licha ya imani hiyo iliyoenea juu ya hatari zinazohusiana na kazi za uchimbaji madini kwa watoto, ushiriki wa watoto katika shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini uliripotiwa kama jambo la kawaida katika jamii za Kerezia, Itumbi na Saza. Wakati wa Majadiliano ya Kikundi (FGD) na mahojiano ya watu wenye ushawishi na viongozi wa jamii, imethibitishwa kwamba ajira za watoto katika migodi zilikuwa ni nyingi kwenye maeneo ya utafiti na watoto wanajiingiza katika shughuli mbalimbali. Hii ilikuwa dhahiri kwa timu ya utafiti wakati wa ziara ya kutazama eneo la utafiti, ambapo watoto wengi na vijana walionekana kufanya kazi katika shughuli mbalimbali za uchimbaji madini.

Washiriki wa utafiti walionesha kuwa shughuli zinazoendelea za uchimbaji madini katika maeneo ya migodi zimeathiri vibaya uamuzi wa watoto wengi kuhudhuria shule. Hii ni kwa sababu, walisema, mtoto akianza kujihusisha na shughuli za uchimbaji madini, huzoea kupata fedha na hii inamfanya kurudi shule kuwa sio kipaumbele chao tena.

Baada ya watoto kuzoea shughuli hizi za uchimbaji madini, huhamasishwa na mapato na pale wazazi wanapojaribu kuwazuia na kuwaambia warudi shulle jibu la ni (EURO) kwanza, kusoma baadaye
- Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanawake, Bukombe

Hawakusikilizi hata kidogo. - Majadiliano ya Kikundi (FGD), Wanaume, Chunya

Maoni hayohayo yalitolewa na watoto ambao hawajishughulishi na shughuli za uchimbaji madini. Baada ya watoto na vijana kushiriki katika migodi, walisema, hawaoni sababu ya wao kurudi tena shuleni.

Wakizoea kupata fedha inakuwa vigumu kuwazuia kufanya kazi na kama utajaribu kufanya hivyo, unaweza kuwasikia wakisema "kwa nini nirudi shuleni? ... Kuna fedha hapa. "
- Kijana asiyefanya kazi katika machimbo ya madini, miaka 15, Songwe

Baadhi ya wachimbaji watoto wenyewe walikuwa na maoni tofauti, ingawa. Wengine wanajikuta wakifanya shughuli za uchimbaji madini kwa sababu hawana namna. Hii ilisemwa waziwazi na wachimbaji watoto wawili, ambao walisema wanafanya kazi katika migodi tu kwa sababu wana shida.

Hakuna kitu kinachonivutia kwenye hii kazi, ninafanya tu kwa sababu ninashida. Na kitu ambacho sikipendi katika shughuli za uchimbaji madini ni kitendo cha kuchimba bila kupata maslahi bora, unachoka au wakati mwingine hupati dhahabu, wakati mwingine hulipwi au unalipwa fedha kidogo kuliko kazi uliyofanya. - Mchimbaji kijana wa kiume, miaka 14, Chunya

Ninafanya kazi lakini sijaridhika na malipo, ninafanya kazi kwa sababu ninashida.

Maoni ya kwamba wazazi na wanajamii kwa ujumla wanakubaliana na ajira kwa mtoto katika maeneo ya mradi yalikuwa mchanganyiko. Baadhi ya washiriki kwenye mahojiano wanaamini kwamba kuna wazazi katika jamii wanaokubaliana na ajira za mtoto. Washiriki walisema baadhi ya wazazi wanawatuma watoto wao kwenda kufaya kazi migodini au wanaridhia kimya kimya.

Wazazi wengine wanawatuma watoto wao kwenda kufanya kazi migodini ili kupata fedha. - Kiongozi wa Jamii 1, Bukombe

Wanawaona watoto wao wakienda huko [migodini] lakini hawasemi chochote, hawajali

- Mwalimu wa shule, Chunya

Wazazi wachimbaji waliamini ajira za watoto hazikubaliki katika jamii; badala yake watoto wanafanya kazi katika migodi bila wazazi wao kujua au ridhaa yao.

Watoto ... wanatoroka nyumbani, wazazi hawajui wako wapi. - Mzazi wa mchimbaji 1, Songwe

Nilijaribu kumzuia kwenda migodi lakini hataki kusikia. - Mzazi wa mchimbaji 2, Bukombe

3.5. Je wachimbaji watoto ni kina nani?

3.5.1. Takwimu

Wachimbaji watoto ni wa jinsia zote wasichana na wavulana na wanaripotiwa kuanza kufanya kazi katika migodi wakiwa na umri wa kuazia miaka 7. Watoto wenye umri mdogo zaidi ya huo wanakuja na mama zao. Muundo wa kaya ya watoto wanaofanya kazi migodini ulikuwa tofauti na yatima, watoto kutoka kwenye kaya zenye mzazi mmoja, na wale wenye wazazi wote wawili hai walijumuishwa na Watoto Walioko kwenye Machimbo ya Madini. Washiriki walisema kuwa katika maeneo ya migodi unawakuta watoto wengi wadogo. Baadhi yao wako pale wanacheza tu wakisubiri wazazi wao wamalize kazi, wakati wengine wako pale kuwasaidia wazazi wao kukusanya mawe.

Unamkuta mtoto anajishughulisha kubeba mawe kwa ajili ya kuyasaga, wakati mwingine wanawasaidia wazazi lakini pia watu huwaomba kuwasaidia kubeba vifaa vyao ama kupeleka sehemu ya kusagia au maeneo ya kuoshea kwa ajili kujipatia fedha kidogo ya kununulia chakula tu, ukimwangalia mtoto ni kama ana umri wa miaka miaka 7 au chini ya hapo.

- Majadiliano ya Kikundi (FGD) ya Wanaume, Bukombe

Watoto wengi wanaofanya kazi zinazohusiana na uchimbaji madini huanza wakiwa na miaka 10, hata hivyo, unawakuta pia wengine ambao wana umri wa chini ya miaka 10 wakifanya kazi kule-baadhi yao hawapo pale kwa ajili ya mtu yeyote, hawachimbi mashimo, lakini wako pale kwa ajili ya maslahi yao wenyewe au wanawasindikiza wazazi wao, na wakati wakiwa pale unawaona pia wakitafuta mawe na kuwasaidia wazazi kubeba mawe kwa ajili ya kuyakata au kupeleka kwenye mashine ya kusagia. Kumwona mtoto wa kiume mweye miaka 7 akibeba debe la mawe kwa ajili ya mzazi wake au mawe ambayo ameyatafuta mwenyewe sio kitu cha kushangaza kule

- Majadiliano ya Kikundi (FGD ya Wanawake, Chunya

Majadiliano ya Kikundi (FGD) na Mahojiano ya watu Muhimu (KII) na watu wenye ushawishi mkubwa yalionesha kuwa baadhi ya hawa watoto walihusishwa na shughuli za uchimbaji madini bado wakiwa na umri mdogo wanapokuwa wanaenda migodini na wazazi wao ambao wenyewe wanafanya shughuli za uchimbaji madini. Kwa mfano, katika maeneo yote, ilionekana kuwa baadhi ya kina mama wanaonyonyesha wanaojishugulisha na shughuli za uchimbaji madini mara nyingi huenda na watoto wao wadogo kabisa na watoto wakubwa kidogo kwenye maeneo ya mgodi. Mtoto mkubwa hutegemewa kumsaidia mama kumhudumia mdogo wage wakati akifanya kazi kwa sababu hakuna mtu wa kumwachia mtoto nyumbani. Kuwepo kwa mtoto katika mazingira hayo kulijulikana kama zoezi la kuyafahamu mazingira kwa mtoto. Hii iliripotiwa kuwavutia baadhi ya watoto kwenye uchimbaji wa madini.

Baadhi ya hawa watoto unaowaona leo katika migodi wamekuwa katika mazingira haya tangu walipokuwa wadogo sana ... Ni kawaida kumwona mwanamke akiwa amembeba mtoto mgongoni akienda maeneo ya mgodi akisindikizwa na mtoto mkubwa kidogo ambaye anaenda kule kwa ajili ya kumwangalia mdogo wake. Mtoto mdogo akiwa amelala, yule mkubwa anaanza kuzunguka akitafuta mawe yaliyotupwa ambayo yanawezekana kuwa na madini. Mawe ambayo mtoto atayapata huongezwa kwenye yale ambayo mama ameyapata na mapato ya siku. Kwa hiyo kadiri mtoto anavyokua inakuwa vigumu kumzuia kufanya shughuli hizo kwa sababu wamekuwa wakifanya hivyo na wazazi wao na bila shaka, ndiyo shughuli pekee waliyoijua ambayo inawaingizia familia zao kipato na kuweza kuishi.

Mazoea ya kina mama ya kwenda na watoto wao kwenye maeneo ya migodi yalitajwa kuwa sio kuwazoesha watoto wao wakubwa tu kujiingiza kwenye shughuli za uchimbaji madini, lakini kunahatarisha afya na maisha ya watoto wao, wakati mwingine husababisha madhara makubwa.

Kulikuwa na tukio moja ambalo mama alienda kwenye machimbo ya madini na mtoto wake. Alimweka mtoto wake kando huku akiendelea kuchagua mawe mazuri. Kadiri mama huyo alivyoendelea na shughuli yake, mtoto alikuwa akitammbaa taratibu, akafika kwenye ukingo wa shimo na hatimaye akatumbukia. Mama alihisi kama kuna kitu kimeanguka alipogeuka kumwangalia mtoto hakumwona wala hakusikia sauti yake tena. Akaanza kulia, watu walipokuja, waliangalia ndani ya mashimo yaliyopo karibu, mtoto alikuwa kwenye mojawapo ya yale mashimo, mtoto alipatikana chini ya shimo akiwa tayari ameshapoteza maisha.

- Mtoa huduma ya afya 2,

Kwa upande mwingine, baadhi ya wazazi wachimbaji walisema wanawahusisha watoto wao katika shughuli za uchimbaji madini ili waweze kupata msaada kwa kile ambacho wazazi hawawezi kukifanya. Mazoea haya yaliripotiwa kama ni tabia iliyozoeleka kwenye utafiti, hasa miongoni mwa kina mama

Ninapoondoka nyumbani kawaida huondoka na mwanangu ambaye ana umri wa miaka 10. Hunisaidia kubeba mchanga, mimi huingia mwenyewe ndani ya shimo na kutoa mchanga nje, kisha hupeleka mchanga kwenye mashine ya kusaga mawe. Baada ya kuyasaga hunisaidia kuyaosha na kutenganisha dhahabu kwa kutumia zebaki, kwa sababu sijui jinsi ya kuosha na kutenganisha.

3.5.2. Mahudhurio ya shule na masomo

Kufanya kazi migodini kuliripotiwa kusababisha utoro, au vyote viwili kuacha shule na kutokuandikishwa. Kuacha shule ilikuwa ni kitu cha kawaida kwa wanafunzi wa shule za sekondari. Pia kuna wale waliomaliza shule ya msingi lakini hawakupata fursa kuendelea na masomo zaidi. Watoto wanaweza kufanya kazi zao wenyewe au kuongozana na wazazi wao.

Watoto wengine wana umri wa miaka 7, unawakuta kule-baadhi yao hata hawakuandikishwa shule, wengine wako darasa la pili, au la tatu lakini hawaendi shule, wanaishia porini, wengine wanajishughulisha wenyewe katika mabowmel... yaani ni kama hivyo wapo tu kule...unawakuta wanafunzi pale, wale waliomaliza shule pia...baadhi yao wanatoka nyumbani wakiwa wamevaa sare za shule kama vile wanakwenda shule lakini wakifika njiani wanabadili nguo na kwenda kwenye machimbo...wanaona kama vile shule inawacheleweshа kupata fedha... watu wakiwaona pale, hawajali, wanaona kama kitu cha kawaida.- Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanaume, Songwe

Ilielezwa kwenye utafiti kwamba wanafunzi wengi hawahudhurii vipindi na/ au wanaacha kwenda shule badala yake wanaenda kufanya shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini. Watoto ambao hawajihusishi na uchimbaji madini ambao kwa sasa wako shule walisema kwamba baadhi ya marafiki zao hawahudhurii shule mara kwa mara na badala yake wanafanya kazi katika migodi. Mahojiano ya walimu wa shule yalithibitisha hili. Walimu walilaani vikali kitendo cha kuwashirikisha watoto katika shughuli za uchimbaji madini. Walisema shughuli zinazoendelea za uchimbaji madini katika maeneo yao ni chanzo kikuu cha ajira za watoto katika jamii na sababu kuu ya utoro na kuacha shule. Uchimbaji madini pia uliripotiwa kuwa na athari mbaya kwenye ufaulu wa wanafunzi kwa sababu ya kutokuhudhuria shule ipasavyo. Iliongezwa kwamba hata kama wanafunzi wachimbaji wakija shule wanakuwa wamechoka sana na kushindwa kuzingatia masomo darasani.

Hawawezi hata kusikiliza kile unachofundisha ... unawakuta wanasinzia darasani ... Mara nyingi nawaita ofisini na ukimuuliza anaanza kusema mwalimu, jana nilikuwa kwenye machimbo, kwa hiyo uchovu wa kufanya kazi katika migodi unamuathiri sio tu kiafya bali pia kimasomo na ufaulu wa shule kwa ujumla. - Mwalimu wa

Tatizo la utoro wa wanafunzi na kwenda kufanya kazi kwenye migodi pia liliripotiwa na wachimbaji watoto wenyewe. Mvulana wa miaka 15, mwanafunzi wa darasa la saba, alieleza jinsi anavyoweza kupangilia muda na kuweza kuhudhuria shule na kufanya shughuli za uchimbaji madini.

Baada ya kurudi kutoka shule saa 8:00 mchana huja hapa kufanya kazi, saa 1:00 jioni huenda nyumbani na kuanza kufanya kazi zangu za shule mpaka saa 5:00 usiku kisha hulala ... Ninachoka, wakati mwingine siwezi kufanya kazi ninazopewa kuja kufanyia nyumbani, na siku zingine siendi shule kwa sababu najikuta nimechoka sana lakini haya ndiyo maisha, inabidi nifanye kazi ili nipate fedha kwa ajili ya kujihudumia mwenyewe na mama yangu, leo sikwenda kwa sababu shule imefungwa,kwa hiyo sasa hivi ninafanya kazi zangu kwa uhuru.
- Mchimbaji kijana wa kiume, miaka 15, Songwe

Walimu wa shule pia walisema kwamba wanafunzi ambao wanajihusisha na shughuli za uchimbaji madini huwa na tabia na mienendo ya ukaidi, tofauti na kile kinachoonekana miongoni mwa wanafunzi wengine, wote kwa wenzao shuleni na walimu.

Tofauti ni kwamba wale wanafunzi wanaofanya kazi katika migodi wanakuwa na tabia mbaya, na huwa wagomvi na wakatili kwa wenzao. Kitu kingine ni kwamba wanakuwa na ujasiri kwa sababu wana fedha kwa hiyo wanajiona kama wako sawa na walimu.

- Mwalimu wa shule, Bukombe

3.6. Sababu na mazingira ya ajira za watoto kwenye migodi

Umaskini ulikuwa ndiyo sababu kuu ya ajira za watoto migodini. Sababu zingine za msingi zilizoripotiwa ni: talaka/kuvunjika kwa ndoa, wazazi kutoa kipaumbele kidogo kwenye elimu, mazingira ambayo watoto wanalelewa, na wazazi kufanya kazi kwa muda mrefu na kuacha watoto wao wajihudumie wenyewe.

3.6.1. Sababu kuu: Umaskini wa kaya

Umaskini wa kaya mara nyingi ulionekana kwenye maeneo mengi kama sababu iliyowasukuma watoto kufanya kazi kwenye migodi. Iliripotiwa kuwa hali ya kiuchumi ya kaya na ugumu wa maisha hushawishi vijana wa kiume na kike kuamua kutafuta kazi kwenye migodi.

Sababu ambayo inawafanya watoto wajiingize kwenye shughuli za uchimbaji madini ni kutokana na ugumu wa maisha na kiuchumi, ni umaskini wa kaya ambao unawalazimisha kuondoka nyumbani, wanataka kupata fedha na kuishi maisha yao.

- Kiongozi wa jamii 5, Chunya

Wanataka kupata kipato ili waishi maisha yao. - Majadiliano ya Kikundi,Wanawake, Bukombe

Wazazi wengine wanashindwa kuwahudumia watoto wao na kuwaacha wajihudumie wenyewe hatimaye huwafanya watoto wao kuacha shule na kufanya kazi ili kuongeza kipato cha familia.

- Kiongozi wa jamii 8, Songwe

Washiriki wa utafiti walisema kuwa idadi kubwa ya kaya, wazazi hawawezi kuwatimizia watoto wao mahitaji ya msingi na, hivyo, watoto wanalazimika kufanya kazi ili wapate kipato kwa ajili ya kujikimu wenyewe. Ilisemwa kwenye Majadiliano ya Kikundi (FGD) kwamba watoto wengi wanaofanya kazi wana uwezo mdogo wa kupata chakula, nguo, vifaa vya shule, na mahitaji mengine, hali ambayo huwalazimisha kutafuta kazi ili wajipatie kipato. Watoto wanafanya kazi ili kujikimu kimaisha ilikuwa ni kauli ya kawaida kwenye utafiti. Hii pia ilithibitishwa wakati wa mahojiano na walimu wa shule, ambao walisema kwamba wanafunzi wengi wanaosoma huku wanafanya kazi wanatoka kwenye kaya maskini.

Baadhi ya watoto hapa, wanaporudi nyumbani kutoka shule hawakuti kitu chochote nyumbani; hakuna chakula, hakuna chochote; kwa hiyo wanaamua kwenda kwenye migodi angalau kupata fedha kidogo ya kununulia chakula. Hii ndiyo hali ilivyo, kaya nyingi hapa ni maskini.

- Mwalimu wa shule, Chunya

Wanafunzi wengi shuleni wanafanya kazi wapate fedha ya kununulia chakula na nguo.

- Mwalimu wa shule, Bukombe

Majibu ya majadiliano na wachimbaji watoto kuhusu kwa nini waliamua kushiriki katika shughuli za uchimbaji madini yalikuwa yanafanana na yale yaliyoripotiwa na washiriki wengine kwenye utafiti.

Niliamua kuja kufanya hii kazi kwenye migodi kwa sababu ya umaskini. Sisi ni masikini, baba yangu ni mgonjwa, na pia ninaishi na bibi na wadogo zangu. Hakuna mtu anayeweza kusaidia familia, wananitegemea mimi. Ninatakiwa kutafuta fedha ili kukidhi mahitaji ya familia ambayo yanajumuisha pia matibabu ya baba yangu ... baba yangu ana kifafa.

- Mchimbaji mvulana kijana, miaka 17, Bukombe

Nilifikiri sipaswi kuwasumbua wazazi wangu kuwaomba fedha. Nikaona ngoja niende kufanya kazi ili niwasaidie kwa sababu hawakuwa na uwezo wa kutosha kugharamia gharama zangu za shule kama vile kununua viatu, sare na mara nyingi hulala na njaa usiku.

- Mchimbaji msichana, miaka 13, Bukombe

3.6.2. Talaka na ndoa kuvunjika

Talaka na/au ndoa kuvunjika imeonekana kwenye utafiti kama mojawapo ya sababu za msingi zinazochangia familia kushindwa kuhudumia watoto wao mahitaji ya msingi, hivyo huwafanya watoto kuamua kwenda kufanya kazi kwenye migodi.

> *Wazazi wangu waliachana, nikabaki na mama yangu pamoja na dada zangu wawili. Tulitakiwa kwenda kuishi na bibi yangu lakini huko hatukukaa kwa muda mrefu, tulihamia hapa. Nilianzia shule ya msingi hapa. Mama yangu alikuwa akifanya biashara ya kuuza mkaa na wali na ndiyo iliyoniwezesha kusoma mpaka kufikia darasa la 5 [umri wa miaka 12]. Kama unavyojua wakati mwingine biashara inaweza kuyumba na hiki ndicho kilichotokea kwetu, wakati mwingine tulikuwa tunalala bila kula kitu chochote. Sikuweza kuvumilia kuendelea na shule. Nilimwona mama yangu akihangaika sana na bado alikuwa akirudi nyumbani mikono mitupu. Ilibidi niamue kufanya kazi ili kumsaidia yeye na dada zangu.*
>
> - Mchimbaji kijana wa kiume, miaka 18, Bukombe

Matukio kama haya sio ya nadra; watoto na vijana wengi wanaofanya kazi migodini wana hali hiyohiyo. Wakati wa majadiliano na watu wenye ushawishi katika jamii, iligundulika kuwa dhahabu inapopungua katika maeneo ya migodi, wanaume wengi huhama na kwenda kutafuta maeneo mapya au maeneo mengine baada ya kupata taarifa nzuri "kwamba kuna dhahabu sehemu fulani." Wanapohama, huacha familia zao. Walisema kuwa wanaume wanapofika maeneo mapya, mara nyingi huanzisha mahusiano mpya na kuanzisha familia, na kusahau kuhusu mke na watoto waliowaacha. Hii ilionekana kuwa ndiyo sababu ya kaya nyingi kuongozwa na wanawake katika jamii za utafiti. Kina mama wanajitahidi kuwalea watoto wao wenyewe kwa hali na mali, na watoto wanapata madhara ya kisaikolojia na kijamii kwa kuwa hawawajui baba zao. Kwa hivyo, walisema, kwa sababu ya ugumu wa kiuchumi haishangazi kumkuta mama na watoto wake wote wakitafuta mawe kwenye migodi.

> *Unamkuta mwanaume ameitelekeza familia yake yenye watoto sita, siyo rahisi kwa mama kwa sababu, unamkuta na watoto wake wote sita*
>
> - Mtu mwenye ushawishi, Songwe

3.6.3. Elimu kupewa kipaumbele kidogo

Majadiliano mengi na watendaji/maafisa wa wilaya, viongozi wa jamii, walimu wa shule, na watu wenye ushawishi katika jamii yalionesha kuwa kuwapeleka watoto shule ni suala ambalo linapewa kipaumbele kidogo na jamii katika maeneo ya migodi. Hii inaweza kuelezewa na tabia ya kuwa na makazi ya muda mfupi na kuhamahama kwa jamii ya wachimbaji na shughuli zao. Wachimbaji wengi huhama hama na makazi yao huwa ya muda mfupi kwa kuwa wanahamia kwenye machimbo mapya porini, ambapo huduma, ikiwa ni pamoja na shule, hamna. Pia, tabia ya kuhamahama ya kundi hili huwafanya iwe vigumu kuwapeleka shule.

> *Elimu inapewa kipaumbele kidogo hapa, kila mtu anafikiria kuhusu dhahabu, wakati mwingine unakuta kaya ambapo wazazi wote ni wachimabji-kuanzia asubuhi mpaka jioni wako porini wanatafuta dhahabu, hawana muda -wanawaacha watoto wajihudumie wenyewe.*
>
> - Mmiliki wa modi 1, Chunya

Mawazo ya kwamba baadhi ya wazazi katika maeneo ya migodi huwashawishi watoto wao wasifanye vizuri kwenye masomo yao shuleni pia yaliibuliwa. Wakati wa majadiliano na walimu wa shule na wanajamii, ilibainika kwamba wazazi huwaambia watoto wao wasifanye vizuri darasani, wakidai kwamba mtoto anapofaulu na kujiunga na shule ya sekondari, wazazi hawana fedha za kuwagharamia. Tabia hii inawakatisha tamaa wanafunzi na kuwafanya wasiongeze bidii kwenye masomo yao na kuwafanya kuzipa kipaumbele kikubwa shughuli za uchimbaji madini kuliko kusoma.

3.6.4. Mazingira ya kijamii ya watoto

Shughuli za uchimbaji mdogomdogo wa madini zimeenea kwenye maeneo yote ya utafiti. Wakazi wengi katika jamii za machimbo ya madini inasemekana ama wanajihusisha na shughuli za uchimbaji

madini kwa sasa au wameshawahi kufanya shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini hata mara moja katika maisha yao. Hakika, walisema kwamba idadi kubwa ya jamii zinazozunguka migodi zimebadilika kwa sababu watu walikuwa wakihamia sehemu hizo ili kufanya shughuli za uchimbaji. Washiriki wa Majadiliano ya Kikundi (FGD) walisema kwamba uchimbaji madini ni shughuli inayothaminiwa na wanajamii wengi wanaamini kwamba uchimbaji madini una mapato makubwa sana.

Majadiliano ya viongozi wa jamii yalibainisha kuwa wazazi katika jamii hawashangazwi kuona watoto wao wakifanya kazi kwenye migodi kwa sababu hii ndiyo njia ya maisha waliyopitia pia. Wanajamii wengi waliripotiwa kuwa wachimbaji wenyewe. Ilionekana kuwa shughuli za uchimbaji mdogomdogo wa madini zinathaminiwa na zinazingatiwa katika maeneo ya utafiti. Wakati wa Majadiliano ya Kikundi (FGD) na Mahojiano ya Kina (IDI) na viongozi wa jamii, walimu wa shule, wamiliki wa migodi, na maafisa/watendaji wa wilaya na Mahojiano ya Watu Muhimu (KII) na watu wenye ushawishi, mara kwa mara ilipendekezwa kwamba mazingira ya kijamii na mazingira ambamo watoto wengi wanalelewa huchangia kwa kiasi kikubwa katika uamuzi wao wa kujihusisha kufanya kazi zinazohusiana na uchimbaji madini. Majibu kama haya "watoto wanaiga kutoka kwa wazazi wao na wanachokiona kutoka kwa watu wengine katika jamii wakifanya" yalikuwa ni majibu ya kawaida.

Familia nyingi katika jamii hii wanajihusisha na shughuli za uchimbaji madini; hii ndiyo shughuli kuu hapa kwa wanaume na wanawake. Hivyo, watoto hujifunza kutoka kwa wazazi wao na kuanza kujifunza kidogo kidogo. Wanaiga kile wanachokiona watu wakifanya katika jamii. Pia [inanishangaza] kuona kwamba baadhi ya wazazi hawajui mahali ambapo mtoto wao yupo, na wazazi wengine wanawaambia watoto wao waende kuwasaidia shughuli za uchimbaji madini; hususan kina mama, hufanya hivi bila kujua kwamba wanawaanda watoto wao kisaikolojia kufanya shughuli hizohizo katika maisha yao baadaye.

Ili kuelewa vizuri mazingira ya familia ya wachimbaji watoto katika utafiti kuhusiana na shughuli za uchimbaji madini, watoto wanaofanya kazi katika migodi waliulizwa nani mwingine katika familia zao hufanya shughuli za uchimbaji madini. Wengi wa wachimbaji watoto walikuwa na angalau mwanafamilia moja kwa sasa au zamani aliyejihusisha na kazi zinazohusiana na uchimbaji madini. Wale watoto wenye wazazi na/au ndugu wanaojihusisha na shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini kwa sasa ama walifanya kazi kwenye migodi hiyo hiyo ambayo familia au katika migodi walikuta jamii nyingine.

Kwa upande mwingine, ilivutia kujifunza kwamba si wazazi wote wanaofanya kazi katika migodi walipenda watoto wao kuwa wachimbaji. Kwa Kerezia, kwa mfano, mmoja wa wazazi wachimbaji alieleza kuwa kazi ya kuchimba madini sio tu ngumu sana kwa mtoto, lakini mazingira ya uchimbaji madini na utamaduni sio kitu chenye manufaa ambapo mtoto anatakiwa kuwepo.

Maoni hayo hayo yalitolewa wakati wa majadiliano na watoto ambao hawajihusishi kwa sasa kwenye migodi. Baadhi ya hawa watoto ambao hawafanyi kazi katika machimbo ya madini waliripotiwa kwamba wazazi wao wamewazuia hata kutembelea maeneo ya mgodi kwa sababu wazazi wanaamini kwamba kama watoto wataruhusiwa kwenye migodi, haitakuwa rahisi kwao kuzingatia masomo yao.

Wote mama yangu wa kambo na baba yangu wanafanya kazi katika migodi, lakini mimi sijawahi kwenda kutembea kwenye migodi au hata kuwatembelea wao kwenye kwenye eneo lao la machimbo ya madini. [Kwa nini?] Kwa sababu baba yangu hataki kuona mtoto wake yeyote akienda au kufanya kazi katika migodi. Ndiyo kwa sababu anasema mtoto akianza kufanya kazi ya uchimbaji madini, itakuwa vigumu kwake kuendelea vizuri na masomo.

- Msichana kijana ambaye hafanyi kazi kwenye machimbo ya madini, miaka 16 (kidato cha 3 shule ya sekondari), Chunya

Matokeo ya mahojiano ya kiongozi wa jamii yalionesha kuwa umaskini wa kaya katika maeneo ya utafiti umesababishwa na hali ya kutokuwa na kipato cha uhakika kwenye kaya. Shughuli za uchimbaji madini ndogondogo ziliripotiwa kama chanzo kikuu cha mapato katika maeneo yote matatu ya uchimbaji madini yaliyotembelewa. Licha ya kuwa na ardhi yenye rutuba ya kilimo, shughuli za kilimo na ufugaji zinachukuliwa kama shughuli za ziada na hufanyika kwa kiwango kidogo. Hii ni kwa sababu ya mtazamo ulioenea katika jamii kwamba mtu anaweza kupata mapato zaidi kwa muda mfupi kwa kufanya shughuli za uchimbaji madini kuliko kupitia shughuli za kilimo kwa sababu shughuli za kilimo

huchukua muda mrefu na hakuna uhakika wa kupata mavuno mazuri. Pindi uzalishaji wa dhahabu unapokuwa mdogo kwa sababu ya kupungua kwa madini kwenye migodi, athari kwenye kaya ni kubwa sana kwa sababu hawana kitu cha kutegemea. Watoto na vijana wadogo wanakuwa wahanga wa hali hii.

3.6.5. Wazazi kuwa mbali na watoto wao kwa muda mrefu

Washiriki katika utafiti waliamini kutokuwepo kwa wazazi nyumbani kuwahudumia na kuwaongoza watoto wao hali hii huwapa watoto uhuru wa kufanya chochote wanachotaka, ikiwa ni pamoja na kujiingiza katika shughuli za uchimbaji madini. Baadhi ya wachimbaji watoto waliripotiwa kujiingiza katika shughuli za uchimbaji madini baada ya kuona wenzao wemejihusisha na hakuna mtu wa kuhoji na kufuatilia mambo yao. Hili lilithibitishwa na mmoja wa wazazi wachimbaji huko Kerezia, ambaye alisema kuwa mtoto wake alianza kutoroka shule na kwenda kwenye shughuli za uchimbaji madini alipokuwa akisafiri mara nyingi kwenda mikoa mingine kwa ajili ya biashara na kwamba hakuwa na muda wa kukaa nyumbani kuwahudumia watoto wake.

Uzalishaji wa dhahabu hapa ulipopungua nilianza biashara ya kununua na kuuza mazao ya kilimo kama vile mahindi, maharage, viazi mviringo, nyanya na kabichi kutoka vijiji vingine na kupeleka Tabora, [mkoa wa jirani]; kama mama, sikuwa na muda wa kukaa nyumbani kwa karibia miezi mitatu. Sikujua kwamba mwanangu aliacha kwenda shule kwa sababu alikuwa akiondoka nyumbani akiwa amevaa sare za shule kama kawaida. Mpaka pale walimu waliponiita na kumuulizia ndipo nikajua kuwa huwa haendi shule. Tulimtafuta tukagundua kwamba alikuwa katika moja ya mwalo wa kuoshea dhahabu; tulimrudisha tena shuleni. Nilijaribu kuongea naye kwa sababu alikuwa anafanya vizuri sana darasani na sikutaka aache shule. Nilimsihi na kumshauri sana kwamba anapaswa kuzingatia masomo kwanza na baadaye atakuja kufanya kazi kwenye migodi. Hata hivyo, aliendelea kutoroka shule na kwenda kwenye shughuli za uchimbaji madini na akaendelea kubadili mwalo kila alipogundua kwamba tunamfuatilia- kwa sababu alikuwa na akili na alikuwa akifanya vizuri sana darasani, walimu wake hawakuniamini mimi kwamba nilikuwa sijui yuko wapi, wao walidhani nimemtuma kwenda kufanya kazi, matokeo yake wakaniweka ndani. Nilikaa pale kwa siku nzima, na walichokuwa wanasisitiza ni kwamba wanataka kujua mwanafunzi alipo na aonekane. Nilichanganyikiwa sio tu kwa sababu ya walimu au kwa sababu niliwekwa ndani bali pia kuhusu mwanangu, kwa bahati nzuri, walimpata kwenye kijiji cha jirani. Ilinibidi niache biashara na kukaa nyumbani muda wote. Sasa hivi tayari yuko darasa la 6, natumaini sasa atatuliza akili yake na kuzingatia masomo yake.

- Mzazi wa mchimbaji 2, Bukombe

3.6.6. Msukumo kutoka kwa wenzao

Msukumo kutoka kwa wachimbaji watoto wengine ambao wanaonekana kuwa na mafanikio katika maisha kwa sababu ya kujihusisha na shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini zinawashawishi watoto kujiingiza katika kazi ya uchimbaji madini. Watoto wanavutiwa na mali zinazomilikiwa na wenzao walizonunua kutokana na kipato kilichotokana na kazi ya uchimbaji madini na wao wanataka kuwa navyo. Waliendelea kusema kuwa baadhi ya hawa watoto sio wote wanaotoka kwenye kaya maskini sana, lakini wanajua hakika kuwa wazazi wao hawawezi kuwapa vitu wanavyotaka na kuvipenda.

Wakati mwingine unakuta hali ya kiuchumi katika kaya zingine sio mbaya sana lakini ni kwa sababu tu mtoto amemwona mwenzake kwa mfano ana simu nzuri, nguo nzuri na ana fedha za kutumia anavyotaka, anaona kama mwenzake amefanikiwa sana na anataka kuwa kama yeye. Kwa hiyo unakuta mwingine anaamua kwenda pia kufanya kazi kwenye migodi ili kupata fedha zake ili awe huru kununua vitu anavyotaka kama wenzake.

- Kiongozi wa jamii 8, Songwe

Ni kama hivyo, unakuta mtoto shuleni hana fedha lakini anaona wenzake wananunua vitafunwa na kula pipi, na vitu kama hivyo, na yeye anajua wazazi wake hawawezi kumudu kumpa fedha za kununulia vitu hivyo. Akifikiria hivyo anaamua kujiunga na wenzake na kufanya shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini ili apate fedha pia. Akirudi shule na fedha na kuwaonesha watoto wengine pia wanavutiwa na kufuata mlolongo huo. Kwa hivyo, mzunguko ni kama huo kwa watoto wengi na matokeo yake unakuta wanafunzi wengi wanafanya kazi migodini.

- Msichana mdogo asiyefanya kazi katika machimbo ya madini, miaka 16 (kidato cha 3 shule ya

sekondari), Chunya

Kitu kingine tunachokiona hapa ni wanafunzi kutaka kuwa na simu za mkononi za kisasa, wanataka kununua simu kwa ajili ya kupiga soga na marafiki zao, matukio hayo yanatokea hapa shuleni na tunawazuia, hivyo unamkuta mwanafunzi hakuja shule badala yake anaenda kufanya kazi katika migodi ili apate fedha za kununua simu ya kisasa na hii ni hata kwa wasichana pia; baadhi yao wanafanya kazi ili wapate fedha kwa ajili ya kununulia vitu visivyo na maana kama hivyo.

- Mwalimu wa shule, Bukombe

3.7. Wachimbaji watoto wanatokea wapi

Idadi ya wachimbaji watoto inaonekana kuwa ya kuhama hama kama kikundi cha watu wazima. Washiriki walisema kuwa Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini (CIM) ni pamoja na wale wanaotoka ndani ya maeneo ya jamii za wachimbaji madini; wale wanaotoka vijiji vya jirani, kata, na wilaya; na wale wanaohamia kutoka mikoa ya karibu na mbali. Walisema kuwa wachimbaji watoto huhamia kwenye maeneo ya mgodi na wazazi wao au huja wenyewe kujaribu bahati zao. Hata hivyo, hakuna mshiriki hata mmoja katika maeneo yote ya utafiti aliyetaja uwepo wa wachimbaji watoto kutoka nje ya nchi.

Wengi wao wamezaliwa na kukulia hapa. - Mtu mwenye ushawishi, Saza, Songwe

Pia, kuna wale wanaotoka vijiji na kata za jirani pia wapo hapa.

- Kiongozi wa jamii 3 Kerezia, Bukombe

Watoto na vijana wanaofanya kazi hapa wanakuja kutoka sehemu mbalimbali za nchi kutafuta maisha.

- Kiongozi wa jamii 4, Bukombe

Katika hii sehemu hapa, unakuta watu kutoka kila mahali, wanakuja kutafuta utajiri, watoto na vijana pia, baadhi yao wamezaliwa hapa, wengine wamekuja na wazazi wao ambao pia ni wachimbaji na wanaishi hapa. Pia kuna wale wanaokuja wenyewe kujaribu bahati zao.

- Kiongozi wa jamii 5, Chunya

Wachimbaji wanahamahama sana, usishangae ukisikia hawa vijana walianza kujiingiza katika shughuli za uchimbaji madini kwa mfano Itumbi leo wako Saza na kesho unasikia wako Nyarlugusu, wanahama kutafuta madini yalipo.

- Kiongozi wa jamii 8, Songwe

Ilifafanuliwa zaidi kuwa uhamiaji wa wachimbaji, ikiwa ni pamoja na vijana, kutoka maeneo mengine kwenda kwenye machimbo umekuwa ni jambo la kawaida kipindi dhahabu inapopatikana kwa wingi kwa sababu maneno ya mdomo yanasambaa haraka. Mfano ulitolewa kwa kurejea machimbo mapya ya madini ya hivi karibuni katika wilaya ya Bukombe.

Taarifa zinaposambaa kuhusu upatikanaji wa dhahabu hapa ndani ya wiki tatu tulikuwa na watu zaidi ya elfu tatu kwenye hili eneo, na baada ya mwezi mmoja, walikuwa zaidi ya elfu tano na hii ni pamoja na vijana wote wavulana na wasichana, wengi wao-utashangaa-wakiwa na simu-ni kama kufumba na kufumbua jicho- taarifa zinasambaa haraka sana na kila mtu anakuwa anakimbilia kuja hapa, hili eneo linafurika watu.

- Afisa wa Wilaya, Bukombe

Dhahabu ikiwa inapatikana huwezi kupata nafasi ya kupita kwenye huu mtaa, unajaa sana watu. Watu kutoka kote nchini wanakuja hapa pamoja na watoto na vijana pia, hii sehemu hufurika, ndipo huona kumbe kuna maisha hapa - Kiongozi wa jamii 2, Bukombe

Viongozi wa jamii waliongeza kuwa baadhi ya watoto wanaokuja baada ya kupata taarifa za upataikanji wa dhahabu bado ni wadogo sana. Wanatoroka nyumbani na wanaweza kukaa hata wiki bila kurudi, mpaka wazazi wao watakapokuja kuwatafuta.

Wengi wao ni wadogo sana huwezi hata kuwaamini kuwa wanaweza kujihudumia wenyewe lakini tayari wameshaingia kwenye shughuli za uchimbaji madini, na wanaweza kutoweka nyumbani hata kwa wiki moja na haijulikani wapi walipo, wazazi wanapata shida kuwatafuta, wakati mwingine wanashindwa kuwapata na kuja kugundua kuwa wako migodini.

- Kiongozi wa jamii 4, Bukombe

3.8. Wachimbaji watoto hukaa wapi

Mahali ambapo wachimbaji watoto wanaishi kwenye migodi hutegemea na jinsi gani walivyofika kwenye eneo la mgodi; Wale watoto wanaoishi karibu na migodi hawahitaji kulala migodini; kwa kawaida hurudi nyumbani baada ya kazi. Watoto hawa hukaa na wazazi au walezi wao ambao wanaishi kwenye jamii ndani au karibu na maeneo ya migodi. Watoto wengi wanaotoka vijiji au wilaya za mbali hukaa ndani ya eneo lao la kazi, kama vile maeneo ya kuoshea dhahabu (mwaloni) au maeneo yaliyo karibu na mashine za kusagia mawe au karibu na mashimo ya mgodi ambapo watu wazima pia hukaa. Baadhi ya vijana inasemekana hukaa na marafiki au ndugu zao ambao ni wenyeji katika jamii hiyo ndani ya maeneo ya mgodi au wamekuwa wakiishi katika maeneo ya machimbo ya madini kwa muda mrefu. Wasichana wengi kutoka maeneo ya mbali wanaripotiwa kukaa sehemu ambayo mabosi zao hukaa. Mawazo ya kwamba baadhi ya wachimbaji watoto hukaa peke yao katika vyumba vya kukodi au kwenye mahema ya plastiki yalisemwa pia. Inaonekana kuwa wachimbaji, ikiwa ni pamoja na watoto na vijana, mara nyingi hupata mahali fulani pa kukaa.

Wengine hukaa ndani ya maeneo ya kusagia mawe ya dhahabu kama wameajiriwa hapo, wengine hukaa ndani ya maeneo yaliyo karibu na mashimo ya migodi, kwa ujumla, hukaa katika maeneo yao ya kazi ... wale wanaotoka maeneo ya karibu hutoka nyumbani kwenda kazi lakini wale wanaotoka mbali lazima wakae pale na wanaweza kukaa popote kulingana na jinsi walivyofika migodi.

-

Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanaume,

Kambi/hema ambapo wachimbaji hukaa

3.9. Utaratibu wa usalama na kushiriki katika kazi za uchimbaji madini

3.9.1. Aina za kazi ambazo wachimbaji watoto hufanya

Watoto na vijana wanaripotiwa kujihusisha na shughuli mbalimbali zinazohusiana na uchimbaji madini, ikiwa ni pamoja na kuchimba na kutoboa mashimo "mafupi" (mapana na yenye kina kifupi) au "mashimo marefu" (mashimo membamba na yenye kina kirefu, wakati mwingine si imara), mashimo, mifuko ya kubebea mchanga wa dhahabu kutoka maeneo ya mashimo mpaka maeneo ya kukaushia na kukata, kupeleka mawe madogo kwenye mashine ya kusaga mawe yenye dhahabu, kusimamia usagaji wa mawe yenye dhahabu kuwa poda, pamoja na kuosha vumbi la dhahabu na maji ili kuishindilia dhahabu. Baada ya kuishindilia dhahabu, kisha wanachanganya unga wa dhahabu uliogandamizwa na maji na zebaki, sasa zebaki hutenganisha chembechembe za dhahabu na mchanga, na kutengeneza aloi ya zebaki. Watoto wakubwa pia wanaripotiwa kuhusishwa na uchomaji wa aloi ya zebaki ili kuvukiza zebaki na kupata dhahabu. Aidha, watoto wanahusishwa na biashara ya uuzaji wa vitu mbalimbali ikiwa ni pamoja na matunda, kuchota maji na kupeleka kwenye migodi. Kwa hiyo watoto wanahusishwa katika nyanja zote za shughuli za uchakataji dhahabu. Binti wa miaka 14 kutoka Songwe ambaye hafanyi kazi kwenye machimbo ya madini alisema kazi hiyo “ni ya kuchosha sana.”

Kazi yangu inahusisha ukataji wa mawe... Ninaanza kwa kukusanya mawe, baada ya

kuyakusanya ninayajaza kwenye gunia na likishajaa ninayakata mawe makubwa vipande vidogo vidogo. Baadaye ninaupeleka mchanga kwenye mashine ya kusaga kwa ajili ya kusagwa ili kupata poda, baada ya kupata dutu ya poda, ninaiosha kwa maji na ile zebaki, kisha ninapata dhahabu. Halafu ninaiuza na kupata fedha. - Mchimbaji msichana mdogo, miaka 13, Bukombe

Wakati mwingine ninachukua mawe kutoka chini, ninapokuwa juu ya shimo kawaida huwa kuna mtu ndani ya shimo ambaye hujaza mchanga kwenye madebe na huwa ninayavuta juu na kumwaga mchanga chini, ninaweza kuvuta kama madebe 50 au 200, na haya madebe, baada ya kusagwa na kuoshwa unaweza kupata karibia pointi 3.1 ya dhahabu [gramu 0.3] kutoka kwenye kila debe ... Kwa kawaida tufanya kazi pamoja kwa kushirikiana watu 2 au watu 3 [wanaofanya kazi pamoja] na wote kwa pamoja tunaweza kubeba karibia madebe 50-70, kuanzia hapo tunakata mawe makubwa kuwa vipande vidogovidogo kabla ya kuyapeleka kwenye mashine ya kusaga ili kupata poda. Baada ya hapo nichanganya hiyo poda na maji na zebaki ili kupata aloi ya zebaki; kisha nakuchukua kipande cha nguo na kukamua zebaki itoke na kupata dhahabu. Huichoma hii aloi ya zebaki ili kuondoa mvuke unatoka na zebaki na kisha tunabaki na dhahabu halisi ya kuuza na kupata fedha. - Mchimbaji kijana wa kiume, miaka 15, Songwe

Mabaki ya mchanga yakikaushwa

Vifusi vya masalia ya udongo yalionekana katika maeneo yote ya migodi yaliyotembelewa. Vifusi hivi viliripotiwa kuuzwa kwa watu wenye "mitambo" ya kuweza kupata dhahabu zaidi, mchakato ambao hutumia sianidi (cyanide). Ilielezwa kwenye utafiti kwamba kwa kutumia zebaki unaweza kupata asilimia 25 tu ya dhahabu iliyopo kwenye mawe, wakati kwa kutumia sianidi (cyanide) mtu anaweza kupata asilimia 75% ya dhahabu iliyobaki. Utayarishaji wa dhahabu kwa kutumia sianidi (cyanide) unahitaji watu wenye ujuzi wa kemikali na mchakato haushirikishi watoto, ingawa baadhi ya wamiliki wa mgodi hufanya kazi kwa kushirikiana na vijana wadogo wa kiume kukusanya mchanga uliyobaki na kupeleka kwenye malori. Wamiliki wa "Mitambo" hununua mabaki ya mchanga na kusafirisha kwa malori mpaka mahali mitambo ilipo. Kuna "mitambo" michache iliyoonekana wakati wa shughuli za ukusanyaji taarifa na hakuna hata mmoja uliyopo ndani ya maeneo ya migodi.

.

3.9.2. Kukosekana kwa usawa wa kijinsia katika shughuli za uchimbaji madini

Ingawa wote wavulana na wasichana wanaripotiwa kufanya kazi katika maeneo ya migodi, hakuna usawa wa kijinsia. Wakati wavulana wanaweza kufanya shughuli zote za uchimbaji madini chini ya ardhi na juu, wasichana wanajihusisha zaidi na shughuli za uchimbaji madini juu ya ardhi, kama vile kuchambua mawe yenye madini, kukata mawe vipande vidogo vidogo na kuyapeleka kusagwa na kwenye maeneo ya kuoshea. Wakati mwingine, wasichana wanajihusisha na shughuli za uchimbaji madini katika migodi mifupi. Ilielezwa kuwa hakuna mwajiri hata mmoja anayewahusisha wasichana katika kuosha na kutenganisha dhahabu kwa kutumia zebaki na kama wasichana wakifanya shughuli hizi, kwa kawaida hufanya hivyo kwa ajili yao wenyewe. Hali hiyo hiyo iliripotiwa kwa wanawake watu wazima katika jamii.

Sababu za kutoshirikisha wasichana na wanawake kwenye uoshaji, kutenganisha dhahabu na mchanga kwa kutumia zebaki, na kuchoma huo mchanganyiko hazikuelezwa kamwe hata baada ya kudodosa. Majibu yao yalikuwa "Ndiyo kama hivyo." Hata hivyo, baadhi ya washiriki walibainisha kuwa baadhi ya watu katika maeneo ya migodi wanachukulia hedhi kama jambo ambalo linaweza kuwafanya watu

wasione madini ya dhahabu. Na, kwa sababu ni vigumu kujua kama wanawake na wasichana wako kwenye hedhi, wanaona ni bora kutowashirikisha kabisa.

Aidha, walisema kwamba wasichana, lakini si wavulana, hufanya kazi kwenye maduka ya vyakula ambapo huandaa na kupika chakula, huuza chakula ama kwa wanajamii wanaoizunguka migodi, au kupeleka chakula kwa watu wanaofanya kazi kwenye mashimo ya migodi porini. Baadhi ya wasichana huajiriwa moja kwa moja na wamiliki wa mgodi kuwapikia watu wanaofanya kazi katika makambi yao. Wasichana pia hufanya kazi kwenye migahawa na baa kama wahudumu wa baa. Iliripotiwa kuwa wasichana hufanya biashara za ngono katika maeneo ya migodi. Mara nyingi wasichana wadogo ambao hufanya biashara ya ngono inasemekana kuwa wanatoka nje ya jamii ya mgodi na hii ilidhaniwa kuwa ni kwa sababu wanataka kupunguza uwezekano wa kufahamika na hivyo hujikuta wakinyanyapaliwa.

3.9.3. Watoto wachimbaji hufanya kazi kwa muda gani

Hakuna muda maalum wa kazi ulioripotiwa kwa watoto wanaofanya kazi kwenye machimbo ya madini. Inasemekana wanafanya kazi muda wowote wakati wa mchana, ama baada ya kutoka shule au siku ambazo wanaotoroka shule (kwa ambao bado wanasoma), na kipindi cha mwisho wa wiki na likizo. Washiriki walisema shughuli za uchimbaji madini hufanywa mwaka mzima. Hata hivyo, mkazo na ukubwa wa shughuli hizo zinatofautiana kati ya vipindi vya kukimbilia dhahabu na wakati wa mvua kubwa. Ilitajwa katika maeneo yote ya utafiti kwamba wakati wa mvua kubwa, shughuli za uchimbaji madini kwenye mashimo marefu husimama na wachimbaji hujikita zaidi kwenye mashimo mafupi na shughuli zingine za uchakataji wa dhahabu.

Kazi kama hizo hazina msimu; zinafanyika kwa mwaka mzima ... wakati wowote unapojisikia, unenda tu kufanya kazi. – Majadiliano ya Kikundi (FGD),Wanawake, Songwe

Wakati wa msimu wa mvua wachimbaji hawaendi kina kirefu ndani ya mashimo kwa sababu mchanga ni mlaini na mashimo yanajaa maji hivyo inakuwa hatari zaidi, lakini wakati wa msimu wa kiangazi kama sasa hivi wanaenda kwenye mashimo marefu na haya hutoa dhahabu nyingi kwa hiyo wanapata fedha zaidi.

- Majadiliano ya Kikundi (FGD), Wanawake, Chunya

Shughuli za uchimbaji madini hazisimami kabisa, utawakuta watu wanafanya kazi muda wote... ni mkazo tu wa shughuli ambao hupungua lakini watu hufanya shughuli za uchimbaji madini mwaka mzima-unapata dhahabu na fedha.

- Majadiliano ya Kikundi (FGD), Wanaume, Bukombe

Kwa hiyo utoro nao huwa hivyo hivyo kulingana na msimu kama ilivyoelezwa na walimu wa shule na wanakikundi kutoka kwenye Majadiliano ya Kikundi.

Wakati wa msimu wa kiangazi, ndiyo kipindi ambacho watoto wengi hawaendi shule kwa sababu wengi wao huenda kufanya kazi katika migodi na hali hii hujitokeza pia kama kuna taarifa kuhusu upatikananji wa dhahabu sehemu fulani.

- Mwalimu wa shule, Bukombe

Mara nyingi watoto hupata vishawishi vya kutoroka shule kipindi cha kiangazi na kwenda kufanya kazi katika migodi kwa sababu katika msimu huo uwezekano wa kupata dhahabu ni mkubwa ... ingawa kuna wale watoto ambao wako migodini muda wote lakini pia unaona sura ngeni nyingi wakati dhahabu inapotikana kwa wingi.

- Majadiliano ya Kikundi (FGD), Wanaume, Songwe

Taarifa kuhusu ni kwa muda gani watoto hujihusisha na shughuli za uchimbaji madini na kama wanachukua likizo yoyote pia zilikusanywa. Ilielezwa kuwa saa za kazi hutegemea na kile ambacho mtoto anafanya na anamfanyia nani. Kwa wale watoto wanaofanya kazi kwa ajili ya wazazi wao na/au ndugu zao, mzazi/jamaa huamua muda wa kwenda kufanya kazi na kumaliza. Ikiwa mtoto anafanya kazi kwa faida yake mwenyewe, hakuna mtu ambaye anadhibiti ratiba ya kazi; ni uamuzi wa mtoto mwenyewe wa kwenda au kutokwenda kazini na muda wa kuanza na kumaliza kazi.

Pia ilitajwa kuwa muda na kipindi cha kufanya kazi kwa mtoto hutegemeana na mtoto kupata mtu wa kumpa kazi ya kufanya. Wale wanaofanya kazi kenye mashine ya kusaga huwa chini ya msimamizi ambaye huandaa ratiba ya kazi kabla. Utaratibu wa kawaida wa siku ya kazi kwenye mashine ya kusaga uliripotiwa kuanza saa 2:00 asubuhi na kumalizika saa 12:00 jioni. Saa za kazi pia hutegemea na kiwango cha uzalishaji wa dhahabu. Wakati wa msimu wa uzalishaji mkubwa wa dhahabu, watoto na vijana hufanya kazi kwa muda mrefu zaidi kuliko msimu wa uzalishaji mdogo; Huhitimisha siku pale kazi inapomalizika au giza linapoingia.

Magunia yakisubiri kusafirishwa

Makubalioano ya kufanya kazi kwa watoto na vijana, sawa na yale ya watu wazima, yanaripotiwa kuwa siyo rasmi na hufanywa na mtu binafsi. Wachimbaji watoto wote waliohojiwa walisema kuwa hufanya kazi kama vibarua kwa makubaliano ya mdomo; hakuna hata mmoja aliyesaini mkataba wowote rasmi na mwajiri wake. Kwa hivyo, mtoto yuko huru kuamua siku ambazo anataka kufanya kazi.

Washiriki wa majadiliano ya kikundi walielezea wasiwasi wao kuwa kuna watoto wanaofanya kazi katika migodi wakati wa usiku, wakisema kuna baadhi ya watoto hutoroka nyumbani kwao usiku wa manane na kwenda kufanya kazi migodini. Watoto hawa waliripotiwa kuchambua mawe yenye dhahabu kwa kutumia tochi kwenye mashimo mafupi ya watu wengine na kupeleka ama kwenye maeneo ya kusagia au kuyaficha mahali fulani. Pale wamiliki wa mashimo wanapokuja kwenye mashimo yao siku ya pili asubuhi wanakuta kila kitu kimechukuliwa. Katika kuelezea hili, washiriki walisema kuwa ni vijana wakubwa kidogo wenye umri wa (miaka 15 na zaidi) ambao kawaida hufanya hivyo. Wanasemekana kuiba mawe yenye madini ama kwa ajili yao wenyewe au wanatumwa na watu wengine kufanya hivyo. Mahojiano na afisa wa wilaya huko Chunya,kwa mfano, alisema kuwa kwa sababu ya udogo wa umbo lao, watu wazima huwatuma watoto kwenda kuiba mawe kwenye mashimo ya watu wengine wakati wa usiku na pale hawa watoto wanapokamatwa na wamiliki, huadhibiwa vikali.

3.9.4. Jinsi wachimbaji watoto wanavyopata kazi migodini

Iliripotiwa kuwa watoto wanaofanya kazi migodini walitafuta kazi wenyewe, na wazazi wao, au kupitia marafiki. Wengi wa wamiliki wa mgodi walisema mara nyingi wanapata maombi kutoka kwa watoto ambao wanatafuta chochote cha kufanya ili kupata fedha. Baadhi yao huja na wazazi wao.

Wakati mwingine mtoto anakuja anasema Baba ninaomba kazi; unapomtazama unahisi kwamba anaweza kufanya kazi kwa hiyo unampa kitu cha kufanya. - Mmiliki wa mgodi 1, Bukombe

Baadhi ya hawa watoto walikuja na wazazi wao kuwasaidia kile wanachofanya lakini kadiri

Wengi wa wachimbaji watoto walisema kuwa kwanza waliingia kwenye machimbo ya madini kwa kutembelea migodi wenyewe na kuuliza watu kama kuna kazi yoyote ambayo wanaweza kufanya.

Nilikuja hapa na kuwauliza watu, 'Je! Kuna kazi yoyote ambayo ninaweza kufanya?' ... kisha nilipewa mawe niyakaushe, nilipata fedha na nikarudi nyumbani.

- Mchimbaji kijana wa kike, miaka 13, Bukombe

Mazoea ya watoto, wote wavulana na wasichana, kutafuta kazi zao wenyewe mara nyingi yaliripotiwa kwenye maeneo yote. Washiriki wa utafiti pia walisema kuwa baadhi ya watoto huingia kwenye migodi wakati wanapoongozana na wazazi wao na/au marafiki ambao pia wanajihusisha na shughuli za uchimbaji madini.

> *Mwanzoni, nilikwenda pamoja na marafiki zangu, nilianza kuwaangalia jinsi walivyokuwa wanafanya ... kisha nikaanza kwenda na kufanya kazi mwenyewe.* - Mchimbaji kijana mvulana, miaka 16,

3.10. Malipo ya kufanya kazi migodini

3.10.1. Jinsi wachimbaji watoto wanavyolipwa

Malipo yanaripotiwa kuwa ya kupatana kati ya mtoto mchimbaji na mtu anayempa kazi kulingana na shughuli inayofanywa. Kama ilivyoelezwa hapo awali, wachimbaji watoto wengi wanajihusisha na kazi ndogo ndogo maalum kama vibarua. Malipo hufanywa baada ya mtoto kumaliza kazi aliyopewa kulingana na makubaliano na hutegemea na bahati ya wachimbaji wa siku hiyo. Hata hivyo, ilielezwa kuwa wachimbaji watoto wanapofanya kazi na wazazi wao, mzazi ndiyo hupatana bei.

Sawa na malipo ya shughuli zingine za uchimbaji madini, malipo kwa watoto wanaofanya kazi kwenye mashine za kusaga mawe yanatofautiana kulingana na mtu ambaye mtoto anamfanyia kazi yake. Hata hivyo, utaratibu wa malipo ni kwa siku, mwezi, au wakati wowote bosi anapokuwa na fedha na nia ya kuwalipa. Pia iliripotiwa kuwa kuna watoto ambao hushirikiana na watu ambao wanamiliki maeneo ya kuosha/kusafishia. Kwa mfano, wanakubaliana kuwa kijana atakuwa na jukumu la kukusanya mabaki ya udongo/mchanga yaliyobaki ili kuyauza kwa wamiliki wa “mtambo” kwa sharti kwamba baada ya mchanga kuuzwa kijana atalipwa kiasi fulani cha fedha. Muda wa chini wa kukusanya mabaki ya udongo unaweza kuwa miezi mitatu na muda wa kusubiri kuuza unategemea na upatikanaji wa mteja. Katika kipindi hicho, vijana waliokusanya na kulundika udongo huo hawapati malipo yoyote. Vijana hawa walisema wanafanya shughuli zingine zinazohusiana na uchimbaji madini, sawa na zile zinazofanywa na watoto wengine, ili kupata kipato kwa ajili ya kujikimu maisha yao ya kila siku.

Pia ilibainika kuwa makubaliano ya mdomo kati ya mtoto na mwajiri wake, yaliandaliwa kwa maslahi ya mwajiri, hamna shahidi na matokeo yake inakuwa rahisi kwa mwajiri kwenda kinyume na makubaliano hayo. Ushahidi huu ulionekana wakati wa Majadiliano ya Kina (IDI) na wachimbaji watoto ambao waliripotiwa kuwa na matatizo mara nyingi kuhusiana na malipo yao, kama vile kulipwa malipo kidogo, kulipwa chini ya kile kiwango walichokubaliana, malipo kuchelewa, au kutolipwa kabisa. Kwa sababu ya umri wao mdogo, hakuna mchimbaji mtoto hata mmoja katika utafiti aliyesema kwamba ameshawahi kutoa taarifa kwenye mamlaka husika kuhusu vitendo hivyo wanavyofanyiwa. Watoto wengi ambao walifanyiwa vitendo hivyo vya dhuluma walisema kuwa waliacha jambo hilo kama lilivyo.

> *Kuna vitendo vingi vya dhuluma hapa hususan vinavyohusiana na malipo, inategemeana na roho ya mtu. Wakati mwingine unampata mtu ambaye anakupa kazi ya kufanya lakini anakupa fedha kidogo au chini ya kiwango tofauti na mlivyokubaliana na wakati mwingine unaweza usilipwe kabisa. Hii imetokea kwangu mara kadhaa, lakini huna la kufanya kama akikudhulumu ... Wakati mwingine waajiri wanakuwa na roho nzuri, wanakuambia wazi kuwa hawakufanikiwa, wakimaanisha kwamba hawakupata dhahabu kwenye kazi uliyoifanya, lakini pia kuna wale ambao wanajifanya hawakupata chochote wakati walipata, wanataka tu kukudhulumu. Kipindi fulani mwaka huu niliosha magunia 15 ya mchanga ya mtu fulani tulikubaliana angenilipa shilingi 1000 kwa kila gunia, jumla Shilingi 15,000, lakini hajanilipa mpaka leo, ni miezi 6 sasa imeshapita na hajasema kitu chochote ninabaki kumtazama siwezi kumfanya kitu chochote kwa sababu ni mkubwa kwangu.* - Mchimbaji mvulana vijana, miaka 18, Bukombe
>
> *Mwajiri ndiye ambaye anaamua kuhusu malipo, kama akiamua kukulipa laki moja au mbili ni uamuzi wake, siwezi kukataa, wakati mwingine analipa 80000/= tu na anaweza kukaa hata miezi mitano bila kulipa hatuwezi kufanya kitu chochote.* - Mchimbaji mvulana kijana, miaka 17, Bukombe

Mzazi mchimbaji wa kike alithibitisha kuwa hakuna malipo maalum yanayotolewa kwa watoto; kimsingi wao hugawana faida.

Mara nyingi hulipwa kulingana na kile kilichopatikana ingawa ni kidogo sana, hakuna kiwango maalum, ikiwa mmiliki anapata malipo zaidi na malipo ya kazi pia yataongezeka kidogo lakini kama mmiliki amepata kidogo, basi na mtoto huwezi kupata malipo mazuri sana. Malipo wanayopata watoto hutegemeana na kile bosi alichopata kutokana na kazi ambayo mtoto alifanya, kama hakukuwa na mapato mtoto hawezi pia kulipwa. -

Mazoea ya kudhulumu malipo pia yaliripotiwa kwa wasichana wanaofanya kazi kwenye migahawa

Baadhi ya kina mama ni wasumbufu sana hasa wakati wa malipo, ninatakiwa kulipwa shilingi 60,000 kwa mwezi lakini anaona vigumu kunipa fedha zote kwa mara moja, ananipa kwa mafungu na kwa kiwango anachotaka wakati mwingine ananipa kama shilingi 2,000 kila siku kiasi kwamba huwezi kuwa na uhakika wa kuipata yote kwa sababu siku nyngine hakupi matokeo yake mwisho wa mwezi ninajikuta sina kitu. - Mchimbaji msichana mdogo, miaka 17,

3.10.2. Kuamua jinsi ya kutumia mapato

Iliripotiwa kuwa wachimbaji watoto wanaofanya kazi kwa maslahi yao wenyewe ndiyo wenye maamuzi na fedha wanazopata na wako huru kuamua jinsi ya kuitumia.

Ninaamua mwenyewe jinsi ya kuitumia fedha kwa sababu ni fedha yangu.
- Mchimbaji msichana mdogo ambaye anafanya kazi katika mgahawa, miaka 17, Chunya

Ni mimi ambaye hufanya maamuzi ya jinsi ya kutumia fedha.
- Mchimbaji kijana wa kiume, miaka 16, Bukombe

Walipododoswa kuhusu ni jinsi gani wanavyotumia fedha, baadhi yao walisema wananunua chakula; nguo, kama vile jinzi nzuri, fulana nzuri, magauni, na viatu; michezo ya video na soka; na vitu vingine kwa ajili ya kusaidia familia zao.

Mimi ninalipwa shilingi 2000 kila siku ... kwa mfano malipo ya leo mama yangu tayari ameniambia ninunue keki ya shilingi 1000 na sukari ya shilingi 1000, nimeshamnunulia tayari na kumpa. - Mchimbaji mtoto mvulana, miaka 12, Chunya

Mimi daima hutuma fedha kwa wazazi wangu na kutumia kiasi kinachobakia kununua chakula na nguo kwa ajili yangu mwenyewe. - Mchimbaji kijana wa kiume, miaka 16, Bukombe

Aidha, wale ambao bado wako shule walisema wanatumia mapato yao kununulia mahitaji ya shule, ikiwa ni pamoja na sare na madaftari ya mazoezi.

Ninaamua mwenyewe jinsi ya kutumia fedha, ninanunua madaftari ya mazoezi, viatu na sare za shule. - Mchimbaji msichana mdogo, miaka 13, Bukombe

Baadhi ya watoto wanaofanya kazi wana mipango ya kutumia mapato yao kujenga nyumba za kudumu au kama njia ya kupata kazi rasmi zaidi, kama vile kuanzisha biashara.

Mimi tayari nimeshanunua kiwanja, sasa nina mpango wa kujenga nyumba yangu mwenyewe.
- Mchimbaji kijana, mvulana, miaka 14, Chunya

Hakika nilihitaji hizi fedha hii kuanzisha biashara, lakini sasa hivi ninashindwa kwa sababu ninapata kiasi kidogo sana ambacho kinatosha tu kwa matumizi ya kila siku; kama ningekuwa na wazazi pengine ningeweza kuweka akiba kwa sababu wangeweza kunisaidia na mambo mengine. - Mchimbaji msichana mdogo, miaka 17, Songwe

Kwa upande mwingine, wanajamii kwenye majadiliano ya kikundi (FGD) waliulizwa watoto hutumiaje fedha zao, wengine walisema kuwa watoto na vijana hutumia fedha kunywea pombe, kuvuta bangi, kucheza pool, kununua simu za kisasa, kuangalia sinema, TV, na kununua vitu vingine vya kifahari. Walisema wasichana hununua vitu vya mapambo kwa ajili ya yao wenyewe.

Tofauti na wachimbaji watoto ambao hufanya kazi kwa ajili yao wenyewe, wale wanaofanya kazi na wazazi na ndugu zao walisema kuwa wana maamuzi kidogo juu ya matumizi ya mapato wanayopata. Baadhi yao walisema hata hawajui kiasi kilichopatikana kwa kazi wanayofanya. Mchimbaji wa kike mwenye umri wa miaka 15 ambaye alihama kutoka kwa wazazi wake baada ya kumaliza elimu yake ya shule ya msingi aliunganana na dada yake ambaye anafanya kazi katika migodi. Alituambia kuwa wanafanya kazi pamoja, lakini hana udhibiti wa mapato. Ingawa dada yake anatumia fedha kununulia chakula kwa ajili ya familia, anafikiri ingekuwa vizuri kama dada yake angempa sehemu ya malipo.

3.11. Sababu za waajiri kuajiri watoto

Kwenye Majadiliano ya Kikundi, waajiri wengi ambao wanaajiri watoto kwa ajili ya shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini walisema wanafanya hivyo kwa sababu watoto ni nafuu na rahisi kuwamudu; hawahoji. Washiriki wengi walisema kuwa watoto ni waaminifu, watiifu, na sio wagomvi sana, kwa hiyo wanapendwa na waajiri wengi. Viongozi wa jamii na watu wenye ushawishi walikuwa na maoni kwamba watu wanawahusisha watoto kwa sababu sio wazuri kwenye kupatana bei, ambapo huwafanya waajiri kuwa na uwezo wa kupanga bei wanayotaka kulipa, kitu ambacho hawawezi kukifanya kwa watu wazima.

> *Ni rahisi kufanya kazi na watoto kwa sababu hawajui jinsi ya kupatana bei na kiwango chochote unachowapa kwao ni kizuri, kwa kuwa wewe ndiyo bosi kwa hiyo unaweza kuamua bei yoyote unayotaka kuwalipa kitu ambacho ni kigumu kama ukifanya kazi na watu wazima.*
>
> - Kiongozi wa jamii 1, Bukombe

Kutaka kuongeza faida pia ilikuwa ni moja ya sababu za kuajiri watoto kwa sababu watoto wanahitaji malipo kidogo na wanaweza kufanya kazi kwa muda mrefu.

> *Wale wanaofanya kazi na watoto wanatafuta faida kubwa kwa sababu wanajua hawa watoto na vijana ni rahisi kuwatumia na wanaweza kufanya kazi muda mrefu kwa malipo kidogo ... kama unavyojua watoto hawafikirii kwa makini na hawafanyi mahesabu wanafurahia tu kiasi wanachopokea. Kwa mfano, unamkuta mtoto amefanya kazi kwa karibu miaka miwili na zaidi na anapewa kitu kama laki nane tu. Kiasi hiki kama kikigawanywa kwa miaka miwili, unakuta malipo ya kila mwezi ni kidogo sana kwa kuwa watoto hawahoji, wanaridhika kirahisi, kwa hiyo kwa asilimia kubwa, watoto hawa hawafaidi kitu chochote, wanawatajirisha waajiri wao.*
>
> – Majadiliano ya Kikundi (FGD) Wanaume,

Washiriki wengine walifikiri kuwa watoto wanaajiriwa kwa ajili ya shughuli zinazohusiana na uchimbaji wa madini kwa sababu wanaweza kubadilika na wanaweza kufanya shughuli ndogo ndogo na kurudia.

> *Unajua tunapofanya kazi na watoto ni rahisi kuwatuma kazi ndogo ndogo .... unajua kwenye machimbo ya madini na sisi pia tunakula, kwa hiyo tunahitaji kupika na vitu kama hivyo, na kama una mtoto kule kwa ajili ya kukusaidia inakuwa rahisi kumtuma, kwa mfano, kuchota maji au kuleta hiki na kile na kama ni msichana, naweza kumwambia apike hata mchuzi, kuosha vyombo na vitu kama hivyo, kazi kama hizi haziwezi kufanywa kirahisi na watu wazima.*
>
> - Mzazi mchimbaji 2, pia mchimbaji, Songwe

Kinyume na kile kilichoripotiwa kwenye Majadiliano ya Kikundi (FGD) na mahojiano mengine, hakuna mmiliki hata mmoja wa mgodi aliyeohojiwa akathibitisha kuajiri watoto kwa ajili ya shughuli za uchimbaji madini. Walisema kuwa watoto ambao wanaonekana wakifanya kazi sasa hivi kwenye migodi hupelekwa na mama zao kuwasaidia shughuli mbalimbali. Walisema, kwa sababu ya hali ngumu nyumbani, kina mama wanapopata fursa ya kufanya kazi katika maeneo ya migodi wanaenda na watoto wao kuwasaidia. Kuna mfano mmoja wa mwanamke aliyeachwa na mume wake. Kwa miaka mitatu iliyopita, amekaa na watoto wake sita na hakuna hata mmoja aliyehudhuria shule. Huyu mama na watoto wake wanaripotiwa kufanya kazi kwenye migodi.

Ilikuwa ni kawaida kwa wachimbaji kusema kwamba sheria ya kitaifa inayoongoza shughuli za uchimbaji madini hairuhusu kumhusisha mtu yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18 katika shughuli za uchimbaji madini na kwamba wanaheshimu sheria hiyo. Baadhi ya wamiliki wa migodi walisema kuwa wale watoto na vijana ambao wanajihusisha na uchimbaji madini hawajaajiriwa; badala yake wanafanya kazi kwa makubaliano fulani kati ya mmiliki wa mgodi na mtoto/kijana.

Wale walioajiriwa hawajaajiriwa moja kwa moja; wanafanya kwa makubaliano kati ya mmiliki wa mgodi na mtoto. Mtoto wa kiume anaweza kupewa kazi ya kuchota maji kutoka mtoni na kupeleka migodini kwa bei ya shilingi 200 kwa ndoo, hivyo kama akibeba ndoo tano kwa baiskeli anapata shilingi 1000- hiyo ni aina ya makubaliano kati ya wamiliki wa mgodi na watoto/vijana ... kwa ujumla katika migodi hakuna kazi zinazofaa kwa watoto, hata hivyo, wakati mwingine unaweza kumkuta mtoto ambaye alikuja kwa sababu ya hali ngumu nyumbani, bila shaka, atapata kazi ya kufanya ili apate kipato kama vile kuosha vyombo ambako anaweza kupata shilingi 1000 -kisha anarudi nyumbani. - Mmiliki wa mgodi 1, Bukombe

Baadhi ya wamiliki wa migodi pia walisema wanawahusisha watoto katika shughuli zao za uchimbaji madini kwa sababu wanawaonea huruma na wanataka kumsaidia mtoto angalau apate fedha kwa ajili ya kununulia chakula au mahitaji ya shule.

Hawa watoto wanakuja kwenye migodi wenyewe, kumbuka wengi wao wanatokea kijiji hiki, baadhi yao wana mpaka umri wa miaka 7 au hata chini ya hapo, huanza kidogo kidogo, wanakuja kuomba kazi yoyote ya kufanya lakini ukiwaangalia jinsi wanayoonekana unawaonea huruma, unaona, kama una kazi yoyote ambayo wanaweza kufanya kama vile kuchukua vitu na kupeleka hapa na pale au kusogeza vitu karibu ... unafanya hivyo ili waweze kupata fedha za kununulia chakula. - Mmiliki wa mgodi 2, Bukombe

Unajua pia wakati mwingine unaweza kumwona mtoto anahangaika kutafuta chakula, yuko pale tu, unaamua kumsaidia kwa kumpa kazi ndogo ndogo za kufanya ili umpe chakula.

- Mmiliki wa mgodi 1, Bukombe

Wakati mwingine tunawapa kazi za kufanya lakini ni kwa ajili ya kuwasaidia kupata mahitaji yao ya msingi kama vile chakula, mavazi na mahitaji ya shule. - Mmiliki wa mgodi 7, Chunya

3.12. Hatari zinazohusiana na kufanya kazi kwenye migodi

Watoto wanaofanya kazi migodini wanakabiliwa na hatari mbalimbali, si tu kwa sababu wanafanya kazi katika mazingira yasiyo salama na bila vifaa vya kuzuia madhara yoyote, lakini pia kwa sababu ya umri wao

3.12.1. Hatari za kiafya

Kuchimba mashimo, kukata mawe, na kubeba magunia mazito ya mawe na mchanga katika mazingira duni yasiyokuwa na vifaa vya kuzuia madhara hizi zilikuwa ni shughuli zilizotajwa zinazoongeza hatari za kimwili kama vile kuumia na maumivu kwa watoto. Washiriki walisema kazi ambazo watoto hufanya huongeza hatari za kupata majeraha na ajali.

Wakati mwingine wanaumizwa na kupoteza maisha kwa kuangukiwa na udongo, kukatwa na mawe, lakini wanaendelea kufanya kazi. - Mchimbaji msichana mdogo, miaka 13, Bukombe

Wavulana wanaripotiwa kuwa katika hatari kubwa ya kuumia kuliko wasichana.

Wavulana huingia ndani ya mashimo; kitendo hiki ni hatari zaidi kuliko kukata mawe ... wavulana wana ujasiri sana na kwa sababu ya asili ya shughuli wanazofanya, wana hatari kubwa zaidi ya kuumia kuliko wasichana. - Mchimbaji mvulana mdogo, miaka 15, Bukombe

Kuwa katika mazingira yenye vumbi, kelele nyingi, na mazingira machafu pia vilitajwa kama hatari za ziada kwa afya ya mchimbaji. Na, wachimbaji watoto wanaofanya kazi katika mashimo ya migodi wako katika hatari kubwa ya kuangukiwa na udongo, mawe au kuteleza kwenye udongo wakati wa kazi. Hatari maalum za mazingira zilizoripotiwa ni kama zifuatazo. Matumizi madogo ya vyoo kwenye maeneo ya machimbo ya madini yaliripotiwa kusababisha matatizo ya tumbo/magonjwa ya matumbo, maambukizi ya njia ya mkojo na homa ya matumbo (typhoid). Kulala nje au chini ya mahema ya plastiki yenye uwazi upande mmoja kulitajwa kuongeza hatari ya kupata malaria na nimonia. Matumizi ya zana nzito na kali kwa muda mrefu kulitajwa kuongeza maumivu ya mgongo, magonjwa ya ngozi, kukohoa, nimonia, na maumivu ya kiuno. Pia waliongeza kuwa watoto wanaofanya kazi katika migodi wako katika hatari kubwa zaidi ya kupata kifua kikuu kwa sababu ya mazingira ya vumbi wanayofanyia kazi. Watoto wachimbaji kuendelea kuwepo kwenye mazingira yenye kelele zinazosababishwa na mashine za kusagia mawe yalitajwa kama kitu ambacho kinaweza kusababisha matatizo ya kusikia baadaye katika maisha yao. Masuala kuhusu hatari za kiafya zinazohusiana na shughuli za uchimbaji madini ilikuwa ikifahamika miongoni mwa washiriki wa utafiti na kwenye maeneo yote.

Wavulana wako katika hatari kubwa zaidi ya kupata ajali na majeraha, wanaweza kujiumiza kwa nyundo au kuumizwa na wenzake, au wakati wako kwenye mashimo wanaweza kuangukiwa na mawe na kupata majeraha na/ au wanaweza kuangukiwa na udongo.
-Mzazi mchimbaji wa kike 2,

Washiriki wote katika utafiti huu, ikiwa ni pamoja na watoto wachimbaji wenyewe, waliona kwamba zebaki ni dutu hatari ambayo ina madhara makubwa kiafya. Hata hivyo, washiriki wengi, ikiwa ni pamoja na watoto na vijana, hawakuweza kutaja njia maalum ambazo zebaki inaweza kusababisha madhara kiafya. Wengi walisema kuwa mtu akitumia zebaki kwa muda mrefu, anaweza kupata maumivu ya mgongo, maumivu ya kiuno, na ugonjwa wa kutetemeka mikono unaposhika kitu. Kwa sababu kuosha na kutenganisha kwa kawaida hufanywa na vijana wadogo wa kiume, iliripotiwa kuwa wavulana wana hatari kubwa zaidi ya kupata madhara ya kiafya kutokana na matumizi ya zebaki kuliko wasichana.

Washiriki walielezea ufahamu wao kwamba matumizi ya zebaki yana athari ambazo huendelea kuathiri mwili wa binadamu kidogo kidogo baada ya muda mrefu. Maoni hayo hayo yalitolewa na watoa huduma za afya ambao walithibitisha kwamba athari za zebaki hazionekani haraka lakini hujikusanya baada ya muda; kwa hiyo, madhara ya matumizi ya zebaki yanaweza kuwa mabaya zaidi kwa mtu mmoja mmoja ambaye alitumia bila vifaa vya kuzuia madhara wakati akiwa na umri mdogo. Watoa huduma za afya walibainisha kuwa zebaki inaweza kuathiri ogani muhimu kama vile ubongo, figo, moyo na mapafu.

Mchimbaji akichenjuaa dhahabu kwa maji na zebaki

Zebaki inatumika sana katika maeneo ya utafiti kwa ajili kuweza kupata chembe chembe za dhahabu. Ilikuwa ni jambo la kawaida katika utafiti kwamba kwa sababu ya athari zake, mtu mwenye jeraha haruhusiwi kuchenjua dhahabu kwa kutumia zebaki. Hii ni kwa sababu ya imani kwamba zebaki husababisha maumivu makali inapoingia kwenye jeraha. Washiriki waliendelea kusema kwamba zebaki inaweza kusafiri haraka sana kupitia jeraha lililo wazi kwenda sehemu zingine za mwili. Waliongeza kuwa, zebaki inapoingia mwilini, mtu huanza kuwa mdhaifu na ukuaji wake huwa si mzuri. Licha ya mitazamo ya kawaida kuhusu madhara mabaya ya kutumia zebaki, lakini bado inatumika sana. Washiriki walisema kuwa zebaki ni nafuu zaidi na inapatikana kirahisi kuliko sianidi (cyanide) na kwamba hawana namna nyingine.

Walipododoswa kuhusu jinsi zebaki inavyoweza kupatikana kirahisi kwenye maeneo hayo, hakuna mshiriki hata mmoja aliyekuwa tayari kuelezea inapatikanaje.

Hatari nyingine ya kiafya iliyoripotiwa ni ile ambayo inahusiana na matumizi ya asidi ya sulfuriki. Huko Saza (Songwe), washiriki wa Majadiliano ya Kikundi (FGD) walionesha wasiwasi wa kutojua nini kitatokea kwao baada ya kutumia asidi ya sulfuriki. Ilielezwa kuwa matumizi ya asidi ni makubwa kwenye migodi na watu wazima na watoto huitumia kusafishia dhahabu chafu. Walisema, asidi inapochomwa, inatoa moshi mwingi na harufu kali. Kwa sababu hiyo, wasi wasi wa washiriki ni kwamba asidi ina madhara makubwa kiafya kuliko zebaki, lakini hakuna hata mmoja aliyeweza kutaja madhara hayo. Washirika wa Majadiliano ya Kikundi (FGD) huko Chunya waliamini kwamba hiyo asidi ina uwezo mkubwa wa kusababisha kansa na inahitaji kuitunza kwa uangalifu wa hali ya juu. Iliongezwa kuwa asidi ikigusa ngozi inaweza kusababisha majeraha makubwa ya kuungua na kama ikiingia moja kwa moja kwenye macho inaweza kusababisha upofu wa kudumu. Mmoja wa washiriki wa Majadiliano ya Kikundi kutoka Kamati ya kata alisema kwamba kama asidi ya sulfuriki ikimezwa, inaweza kuharibu viungo vya ndani na inaweza pia kusababisha kifo. Licha ya hatari inayojulikana inayotokana na matumizi ya asidi ya sulfuriki, bado asidi hutumiwa na vijana na watu wazima katika uboreshaji wa dhahabu kwenye migodi. Kuna ushahidi mdogo kuhusu matumizi ya mavazi ya kukinga madhara, kama vile glovu, mabuti, aproni, na ngao za uso, wakati asidi ya sulfuriki inapotumiwa.

3.12.2. Hatari za kijamii

Kulikuwa na uelewa wa kawaida miongoni mwa washiriki wa utafiti kwamba kufanya kazi katika mgodi hakufai kwa watoto si tu kwa sababu ya umri wao na kiwango cha ukomavu, lakini pia kwa sababu ya hatari za kijamii zinazohusiana na kazi. Hata hivyo, kwa sababu zilizozotajwa katika sehemu zilizopita, watoto na vijana wanalazimishwa kutafuta maisha kwenye migodi. Kwa kufanya hivyo, watoto wanajikuta wanafanya kazi katika mazingira magumu pamoja na watu wazima na kuiga mitindo fulani ya maisha inayohusiana na kambi za uchimbaji madini.

> *Mazingira katika maeneo ya machimbo ya madini yanatisha, magumu na ni mabaya sana kwa watoto na vijana; watu katika migodi wanaishi kama sio wanadamu na watoto wanalazimika kuishi kama wao, wanalazimika kuishi kama watu wazima.*
>
> - Mzazi mchimbaji 1, Bukombe

Ilifafanuliwa zaidi kuwa watoto na vijana katika migodi wanaona vitendo vya watu wazima. Unywaji pombe, kucheza pool na uvutaji bangi inasemekana kuwa ni kawaida katika maeneo ya mgodi. Kuna imani kwamba kuvuta bangi kunamwezesha mtu kuwa mchangamfu na nguvu ndiyo maana wanavuta bangi katika maeneo ya migodi. Katika maeneo yote matatu yaliyotembelewa, uvutaji bangi na ulevi wa pombe viliripotiwa kuwa ni vitu vya kawaida miongoni mwa vijana, ambavyo huathiri sana wachimbaji watoto na jamii zinazozunguka kwa ujumla. Wachimbaji watoto wa kiume waliripotiwa kuwa wana uwezekano mkubwa zaidi wa kujihusisha na uraibu; wanaweza kushawishiwa kuamini kwamba unaweza kuwaongezea nguvu na kumfanya mtu apate ari ya kufanya kazi

> *Kutokana na hali na mazingira wanayoishi katika maeneo ya machimbo ya madini inakuwa ni rahisi kwa vijana wa kiume kuiga tabia mbaya kutoka kwa watu wazima na wenzao kama vile kuvuta bangi na kunywa pombe katika maeneo hayo.* – Mzazi mchimbaji 1, Chunya

Vitendo vilivyofanywa na wachimbaji katika jamii pia viliripotiwa kushawishi tabia za watoto nje ya maeneo ya migodi. Katika moja ya shule, kwa mfano, mwalimu mkuu alitoa taarifa kuhusu tukio la mtoto wa shule ya awali ambaye alikuwa akienda darasani akiwa amelewa na mvulana mwingine wa darasa la pili ambaye alizoea kuvuta sigara. Watoto hawa walipoulizwa walijifunzaje kuvuta sigara na wapi wanapozipata, wote walisema wamejifunza na kuzipata kutoka nyumbani. Tabia za aina hii zinaweza kuwa na madhara makubwa kimaadili na kisaikolojia na zinaweza kusababisha changamoto kubwa ya kuwarekebisha watoto na vijana kadiri wanavyoendelea kukua.

3.12.3. Ukatili na unyanyasaji wa kijinsia

Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa unyanyasaji wa kijinsia hutokea migodini na kwenye jamii za wachimba madini, ingawa suala hilo halizungumzwi waziwazi. Baada ya kudodosa, washiriki wengi wa

Majadiliano ya Kikundi (FGD) walisema kwamba ulevi wa pombe, uvutaji bangi na unyanyasaji wa kijinsia hauwezi kuepukika. Vijana wa kike mara nyingi walikuwa wakidhaniwa kuwa katika hatari kubwa ya kufanyiwa ukatili na unyanyasaji wa kijinsia zaidi kuliko wavulana. Wasichana wanaripotiwa kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji katika shughuli zao za kila siku kwenye migodi kwa kutukanwa matusi, unyanyasaji wa kimwili au unyanyasaji wa kijinsia. Katika hali nyingine, wasichana waliripotiwa kufanya ngono na wateja wa bosi zao ili kutowapoteza wateja wao. Jambo hili lilitajwa mara kwa mara kuwa hutokea miongoni mwa wasichana ambao wanafanya kazi kama wahudumu wa baa na mama lishe. Iliripotiwa zaidi kwamba wasichana wanapotaka kuongeza kipato chao, pia wanaweza kuamua kufanya ngono kwa malipo. Kila jamii ilitaja tukio la msichana ambaye alifanyiwa kitendo cha unyanyasaji wa kijinsia. Kila mwalimu wa shule alielezea uwepo wa watoto wa shule ambao walikuwa wamebakwa. Majadiliano na wazazi wachimbaji pia yalithibitisha kuwa mtoto wa kike anaweza kuteswa na kunyanyaswa katika migodi. Mmoja wa wazazi wa wachimbaji madini huko Itumbi alisema kuwa hatari kubwa za ubakaji katika migodi imesababisha wazazi wengine kuongozana na watoto wao wa kike kwenye migodi na kukaa nao pamoja wakati wa kufanya kazi. Alisema kuwa wachimbaji watoto wa kike hubakwa katika migodi wakati watoto wa kiume hupigwa na kunyang'anywa mali zao, kama vile mawe yenye madini na mchanga.

Bughudha ... Siwezi kukataa, sio tu kwa watoto hata kwa wanawake watu wazima tunazuiliwa kuchimba sehemu zingine na wakati mwingine tunanyang'anywa mawe yetu, tunapoanzisha shimo na wakagundua kwamba lina mawe hutufukuza, wanajua hatuwezi kuwafanya kitu chochote... hata watoto wanabughudhiwa; Kwa kweli sijui hata niseme nini, mazingira haya tunayoishi ni hatari, ni magumu, ndiyo maana tunaamua kwenda pamoja na watoto wetu wa kike, tunakaa na kurudi nao, wasichana wengi wanabakwa na wavulana hupigwa, na kama mtu akigundua kuwa mawe yanaweza na dhahabu yanaweza kuibwa au kunyang'anywa, na huwezi kudai, yote haya tunamwachia tu Mungu. - Mzazi mchimbaji 1, Chunya

Walipododoswa kama wamewahi kushuhudia unyanyasaji wa kijinsia, wazazi wachimbaji wachache walitaja matukio mengi.

Ndiyo, nimeshuhudia matukio mengi sana [waliobakwa], sio wasichana tu bali pia wanaume wanalawitiwa na wanaume wenzao. Kulikuwa na kipindi ambapo walimnunulia pombe mwanaume mmoja na baada ya kulewa wakamfanyia kitendo kibaya. Watu walichanga fedha kumpeleka hospitali ya wilaya lakini baadaye akapoteza maisha. - Mzazi mchimbaji 2,

Majadiliano ya Kikundi yalibainisha kuwa matukio mengi ya ubakaji hayaripotiwi polisi. Hata waathirika wachache ambao wanaripotiwa hawahudhurii mahakamani. Watendaji wa wilaya na viongozi wa jamii walikuwa na maoni kwamba kesi nyingi za ubakaji zinatatuliwa katika ngazi ya familia ama mhusika kuwalipa wazazi na/au walezi kiasi fulani cha fedha au kulazimishwa kumoa mtoto. Ukubwa wa tatizo hili, afisa wa ustawi wa jamii huko Chunya alisema kuwa katika kipindi cha miezi sita (Januari hadi Juni 2017), wilaya tayari imeshafungua mashauri ya kesi 17 mahakamani ya wasichana ambao wamebakwa na kesi tano za wavulana ambao wamelawitiwa. Katika maeneo yote ya utafiti, hofu ya ubaguzi na unyanyapaa ilitajwa kuwa sababu ya kutotoa taarifa za kesi za ubakaji mahakamani.

3.13. Uwepo na upatikanaji wa huduma katika maeneo ya migodi

Uwepo wa huduma za kijamii katika maeneo ya migodi ni mdogo, na, pale zinapopatikana, hakuna huduma yoyote inayowalenga watoto wanaofanya kazi katika migodi. Hakuna eneo hata moja lililokuwa na kituo cha polisi, maji ya bomba, au vyoo. Badala yake, maji huletwa kwenye madumu na watu hujisaidia na kukojoa kwenye vichaka vya maeneo yanayozunguka mgodi.

3.13.1. Upatikanaji wa shule

Upatikanaji wa shule unatofautiana katika maeneo yote. Huko Saza (Songwe), shule ya msingi na sekondari haziko mbali na jamii. Huko Itumbi (Chunya), shule ya msingi iko umbali wa kilomita 2 kutoka kwenye jamii ya wachimbaji madini, na kule Kerezia (Bukombe), ni umbali wa kilomita 4. Kote Itumbi na Kerezia hakuna shule ya sekondari katika jamii ya wachimbaji madini.

Walimu wa shule waliohojiwa katika utafiti walisema huwa wanashiriki katika kuhamasisha wanajamii na watoto wenye umri wa kwenda shule ambao ama wako shule au bado hawajaandikishwa kuhusu madhara ya ajira za watoto katika migodi wakati wowote wanapopata nafasi. Itumbi, kwa mfano, mwalimu wa shule alisema alihudhuria mikutano ya kijiji ili kuhamasisha juu ya tatizo la ajira za watoto na madhara yake ya muda mrefu miongoni mwa watoto wenyewe na jamii kwa ujumla. Kwa kuongeza, kamati za elimu za kata zinaripotiwa kufanya kazi kwa kushirikiana na walimu wa shule katika vijiji husika ili kukabiliana masuala ajira za watoto.

Maafisa elimu wa kata walioshiriki katika utafiti walisema kwamba walipogundua idadi kubwa ya utoro shuleni, waliandaa mikutano maalum kwa kushirikiana na walimu wa shule ili kujadili na wazazi husika kwa nini watoto wao hawahudhurii shule. Ingawa jitihada hizo zinaonekana kama ni muhimu katika kupunguza tatizo la utoro shuleni, walimu wa shule katika utafiti walikuwa na maoni kwamba ajira za watoto katika migodi bado ni tatizo kubwa la kijamii katika maeneo ya utafiti.

3.13.2. Upatikanaji wa huduma za afya

Upatikanaji wa huduma za afya ni mdogo katika maeneo ya utafiti; kituo cha kutolea huduma za afya kilipatikana katika jamii ya Saza (Songwe) tu. Kituo cha kutolea huduma za afya cha karibu kwa KereziaKerezia (Bukombe) na Itumbi (Chunya) kilikuwa umbali wa kilomita 13.

Washiriki wa utafiti walisema kuhusu upatikanaji wa vituo vya kutolea huduma za afya na gharama zake zinazohusiana na usafiri kama kikwazo kwa wanajamii kutafuta huduma za afya haraka, ingawa usafiri haukuripotiwa kama kikwazo cha kupata huduma katika eneo la Songwe.

Washiriki katika maeneo yote walisema gharama za kumwona daktari, vipimo vya maabara, na matibabu ni kikwazo cha kupata huduma za afya haraka na kwa ufanisi. Ilifafanuliwa kwamba mara nyingi vituo vya kutolea huduma za afya havina dawa na wengi hupewa karatasi na kwenda kununua dawa kwenye maduka ya dawa. Ilibainika kuwa watoto wenye zaidi ya miaka 5 na vijana wanatakiwa kulipia huduma zao za afya. Watoa huduma za afya walielezea kuwa hii hutokea tu kama hawajajiunga na bima ya afya. Kwa mujibu wa sera ya afya, watoto chini ya miaka 5 tu, wanawake wajawazito (kwa ajili ya magonjwa yanayohusiana na ujauzito), wazee, na wale wenye magonjwa sugu wanapaswa kuhudumiwa bure. Hata hivyo, mara kwa mara ilibainika kuwa hakuna mwanajamii yeyote aliyekataliwa kupewa huduma za afya alipohitaji kama hawezi kulipia huduma mara moja. Badala yake, wafanyakazi wa afya wanasema, kama mtu hana fedha ya kulipa hapo hapo, mara nyingi huwahudumia kwanza wagonjwa ili kuokoa maisha yao na baadaye hujadiliana na wagonjwa au ndugu zake kuhusu jinsi ya kupata fedha kwa ajili ya kulipia huduma.

Duka la dawa muhimu

Matumizi ya dawa kutoka kwenye maduka ya dawa yaliripotiwa katika utafiti kama kimbilio la kwanza mtu anapougua. Washiriki, watu wazima na watoto, walieleza kuwa wanatembelea vituo vya kutolea huduma za afya pale tu hali inapokuwa mbaya. Maduka yanaripotiwa kuwa na dawa za kutuliza maumivu na kiua vijasumu (antibiotics), na kuonesha matumizi makubwa ya kiua vijasumu (antibiotics) katika maeneo ya migodi. Baadhi ya maduka pia yanaripotiwa kuwa kutoa huduma ya kuchoma sindano kwa wagonjwa wanapohitaji. Kuhusu huduma za kinga, washiriki walisema hununua kondomu na vyandarua kwenye baadhi ya maduka yaliyopo. Iliripotiwa kuwa mara nyingi mchimbaji mtoto anapougua hujigharamia wenyewe huduma za matibabu kama wanaweza, au gharama hulipwa na wazazi au ndugu kama mtoto hana fedha.

Ninapokuwa mgonjwa ninajinunulia dawa mwenyewe kama nikiwa nina fedha. Ikiwa sina fedha, mjomba yangu huninunulia. - Mchimbaji kijana wa kiume, miaka 17, Bukombe

Nilikuwa nina homa, baada ya kutumia Panadokutoka kwenye lile duka sikupata nafuu, ndipo mama yangu akasema kwamba twende zahanati ya Matundasi lakini tulipofika daktari alituambia twende hospitali ya Chunya, tulikwenda kule na baada ya kupima alisema nilikuwa na homa ya matumbo (typhoid) na malaria, mama alilipa gharama na tukarudi hapa.

Wakati mwingine, walisema bosi wao huwalipia gharama za matibabu.

Ikiwa mtu ameajiriwa na akapata bahati ya kuwa na bosi mwenye roho nzuri anaweza akamlipia gharama za matibabu ikiwa ataugua. Hiki ndicho kilichotokea kwa rafiki yangu ambaye anafanya kazi ya kusaga mawe, alipokuwa na malaria bosi wake alimnunulia dawa. - Mchimbaji kijana wa kiume, miaka 17,

Kama mtoto mchimbaji ambaye hana wazazi au ndugu akiugua na hawezi kumudu gharama za matibabu yeye mwenyewe, wachimbaji katika eneo hilo humchangia huyo mtoto ili apelekwe hospitali.

Inatokea unamkuta mtoto ni mgonjwa lakini hakuna mtu wa kumhudumia. Hivi karibuni kulikuwa na mtoto mgonjwa ... umri wake ni karibia miaka 14, alipata homa na alikuwa akitetemeka. Alisema alikuwa ametumia Panado lakini hakupata nafuu. Watu hapa walimchangia fedha ili aende hospitali ... Watu wote wanaofanya kazi hapa [walimchangia], na kuna kitabu ambacho kila mtu ambaye huchangia jina lake na kiasi alichochangia kinaandikwa. Hivyo ndivyo jinsi tulivyopata fedha na yule mtoto akapelekwa hospitali. - Mzazi

Watoa huduma za afya walisema kuwa hakuna kituo hata kimoja kinachotoa huduma maalum kwa watoto wanaofanya kazi migodini. Wafanyakazi wa kituo cha kutolea huduma za afya walisema walimhudumia kila mtu anayekuja kwenye kituo chao. Kuwa karibu na migodi, hii inajumuisha watu wanaotoka kwenye jamii za wachimba madini, lakini ni vigumu kwa watoa huduma za afya kutambua kama mgonjwa anafanya kazi katika migodi. Kwa hiyo, hakuna kinga au tiba maalum inayotolewa kwa watoto katika jamii za wachimba madini.

3.13.3. Mitazamo kuhusu VVU/UKIMWI na upimaji wa VVU na matibabu

Washiriki wengi wa utafiti walisema kuwa VVU/UKIMWI umeenea katika maeneo ya utafiti. Tabia na vitendo vya watu wanaofanya kazi katika migodi vilidhaniwa kuchochea kuenea kwa kiwango kikubwa cha VVU katika eneo hilo. Wasichana wadogo wanaripotiwa kuwa katika hatari zaidi ya kupata maambukizi ya VVU, katika misimu yote ya uzalishaji mkubwa na mdogo ya dhahabu. Wanaume wengi watu wazima wanapenda kuwa na mahusiano na wasichana wadogo kutokana na dhana kwamba wasichana wadogo hawajaambukizwa VVU. Inasemekana wanaume watu wazima wanatumia fedha zao kuwarubuni wasichana wadogo kwa lengo la kufanya nao ngono. Katika maeneo yote, biashara ya ngono ilionekana kama shughuli ya kawaida kwa wasichana ambao wote wanaotoka ndani ya jamii za wachimbaji madini na kutoka maeneo mengine.

Idadi kubwa ya watu wenye tabia na asili tofauti na biashara ya ngono kwenye maeneo ilidhaniwa kuchangia kuenea kwa VVU katika jamii za wachimba madini. Ilielezwa kuwa watu wengine ambao wamekutwa na maambukizi ya VVU hawaamini kwamba wameambukizwa; badala yake wanafikiria kuwa wana hali nyingine au wamelogwa. Mawazo ya kwamba watu wanaacha kumeza vidonge vya kufubaza virusi vya UKIMWI (ART) kwa sababu ya dawa za kienyeji yalielezwa. Mitazamo kama hiyo ya kuhusisha dalili za VVU na ushirikina na imani kwamba VVU inaweza kudhibitiwa kwa matumizi ya dawa za kienyeji ilikuwa ni sababu nyingine iliyochochea kusambaa kwa maambukizi ya VVU.

Takwimu za VVU na UKIMWI maalum kwa jamii za wachimba madini hazikupatikana wakati wa utafiti. Taarifa pekee iliyopatikana ni kiwango cha mjumuisho wa upimaji VVU katika wilaya (kutoka katika mfumo wa serikali wa DHIS-2) ambazo zilionesha kiwango cha kuenea VVU kwa 5.7% kwa Bukombe na 7.1% kwa wilaya za Chunya na Songwe kwa pamoja. Kiwango hiki kinajumuisha upimaji VVU wa idadi ndogo ya watu kwa hiyo haiwezi kuchukuliwa kama kiashiria cha kuaminika cha kuenea kwa VVU katika maeneo ya wachimba madini, kwenye idadi ndogo tu ya watoto/vijana katika maeneo ya machimbo. Taarifa maalum ya maeneo ya migodini itakusanywa kwa njia ya kujaza dodoso wakati wa shughuli za ukusanyaji taarifa za awali za utekelezaji wa mradi wa Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini (CIM).

Kudodosa jinsi watu wanavyojilinda dhidi ya maambukizi ya VVU kumebaini kuwa kuna matumizi madogo ya kondomu katika maeneo hayo. Baadhi ya washiriki wengine wa Majadiliano ya Kikundi (FGD) walibainisha kwamba wanaume wengi wako tayari kutoa fedha zaidi ili wafanye ngono bila kutumia kondomu. Hii ilithibitishwa na mmoja wa wazazi wachimbaji ambaye ana duka katika jamii, aliposema kuwa katika duka lake kondomu ni moja ya bidhaa inayouzika taratibu sana.

Watoto na vijana walioshiriki katika utafiti walidodoswa kama wamepata ujumbe wa VVU/UKIMWI na kama wamewahi kupima VVU/UKIMWI. Wote walisema wamewahi kusikia kuhusu VVU, na wengine walisema kuwa wameshawaona au wanawafahamu watu walioathirika, lakini hakuna hata mmoja aliyesema kuwa ameshapimwa VVU. Maswali kuhusu kwa nini hawakupima hayakutolewa majibu. Watoa huduma za afya, kwa upande mwingine, walisema kuwa kuwapima watoto na vijana VVU/UKIMWI ni changamoto kubwa. Kwanza, kundi la umri huu halina uelewa wa kutohsa kuhusu hatari na madhara ya VVU kwa hiyo hawawezi kupima kwa hiari yao kwa kuogopa kunyanyapaliwa. Pili, walisema, kwa mujibu wa maadili na sheria kuhusu taratibu za kitaifa za kupima VVU na huduma za ushauri, watoto chini ya miaka 18 wanaweza kupimwa VVU/UKIMWI kama wamesindikizwa na wazazi au walezi wanaotambulika kisheria kwa ajili ya kutoa ridhaa. Masuala haya yalielezwa kuwa yanaonekana kunyima uhuru wa kuwapima VVU vijana wadogo.

Vituo vya kutolea huduma za afya hutoa huduma za ushauri kuhusu VVU, huduma na matibabu, na kuzuia maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto katika wilaya zote tatu. Kupunguza matatizo ya upatikanaji wa huduma za upimaji VVU na kuhamasisha kuendelea na matumizi ya dawa, huko Itumbi (Chunya), hospitali ya wilaya hutoa huduma za kutembelea kwa ajili ya kutoa vidonge vya ART kwa jamii iliyo karibu na migodi. Hii imetajwa kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa wengi wanaohitaji. Hii ni muhimu kwa sababu asili ya kuhamahama ya wachimbaji madini, ikiwa ni pamoja na watoto na vijana, ilitajwa kama kitu ambacho kinaweza kufanya matumizi ya dawa za VVU na huduma endelevu kuwa vigumu.

Vikundi vya kusaidia vijana pia vilianzishwa katika maeneo mawili. Huko Bukombe, kuna vikundi vya vijana wanaoishi na VVU, ambapo vijana hutoa msaada wa kijamii na wa kimaadili. Vikundi ya Vijana Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (ALWHIV) pia vilielezwa kuwawezesha vijana kubadilishana uzoefu wao kuhusu kuishi na VVU na kupeana moyo juu ya matumizi na kuendelea kutumia dawa. Kikundi cha vijana huko Saza sio maalum kwa wale wanaoishi na VVU; bali kinalenga katika afya ya uzazi, ambapo masuala ya kujitambua, mimba za utotoni, na kujikinga na magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya ngono, ikiwa ni pamoja na VVU na UKIMWI, yanashirikiwa na kujadiliwa.

3.14. Mipango/miundo iliyopo kwa ajili ya kuwasaidia Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini

Kuna mipango au miundo kadhaa iliyopo tayari kushughulikia suala la ajira za watoto katika migodi, ingawa kwa sababu ya udhaifu wa utekelezaji, tatizo linaendelea kuwepo.

3.14.1. Kamati za elimu za kata

Kwenye kila kata katika maeneo ya utafiti, kuna kamati ya elimu ya kata ambayo inashirikiana na walimu wa shule kufuatilia utoro wa shule na wanafunzi wanaoacha shule katika maeneo yao husika. Washiriki wa utafiti walibainisha kuwa mtoto asipohudhuria shule mara nyingi, kamati ya elimu ya kata kupitia mwalimu mkuu wa shule inawaita wazazi wa wanafunzi kutoa maelezo kwa nini mtoto wao haudhurii shule. Utaratibu huu uliripotiwa kuwepo hata kwenye maeneo ambayo hayana shule karibu.

Kama wazazi, tunapokea barua na wakati mwingine ujumbe wa simu kutoka kwa walimu wa shule wakituita kwa ajili ya mikutano kama wakiona mtoto hahudhurii shule mara kwa mara. Unapotembelea shule, unajadiliana na walimu na maafisa wa kata kuhusu kwa nini mtoto wako hahudhurii shule. Baada ya hapo, walimu na maafisa wanakushauri jinsi ya kumzuia mtoto kwenda kufanya shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini. - Mzazi mchimbaji 2,

Kamati pia iliripotiwa kuandaa ziara ya kushtukiza katika maeneo ya uchimbaji madini pale walipoona kiwango kikubwa cha utoro na kuacha shule kimeongezeka. Katika ziara hizi, watoto wenye umri wa kwenda shule hukamatwa na kurudishwa shule.

3.14.2. Sheria ndogo

Kila eneo lina sheria zake ndogo zinazokataza wamiliki wa migodi kuwahusisha wanawake wajawazito na watoto wenye umri chini ya miaka 18 katika shughuli zao za uchimbaji madini. Baadhi ya wamiliki wa migodi huweka mabango kwenye maeneo yao yakisomeka "ni kinyume cha sheria kwa watoto na wanawake wajawazito kuingia eneo hili." Aidha, sheria ndogo za madini zinaeleza dhahiri kwamba hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wamiliki wa mgodi ambao wanawahusisha watoto na wanawake wajawazito na leseni zao za madini zitafungwa. Hata hivyo, usimamizi mdogo wa sheria ndogo zilizopo ulitajwa kuwa miongoni mwa sababu za utekelezaji duni.

3.14.3. Mipango ya ulinzi ya kifedha

Fedha za msaada wa watoto/jamii

Iliripotiwa kwenye utafiti kuwa kila wilaya hutenga asilimia 5 ya jumla ya makusanyo ya mapato kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya watoto na vijana. Mfuko huo unasimamiwa na wilaya kupitia ofisi ya maendeleo ya jamii. Ilielezwa kuwa ni wajibu wa maafisa wa maendeleo ya jamii kuwafahamisha watu katika wilaya husika kuhusu upatikanaji wa fedha na kuhamasisha watu kujiunga na vikundi ili kuzipata. Kikundi kimoja kinaweza kuchukua mkopo hadi wa shilingi milioni 5 na kiwango cha riba ni asilimia 5.

Wanawake wenye umri wa miaka 15-55 na wanaume wenye umri wa miaka 18-35 wanastahili kupata mkopo kutoka kwenye mfuko huo. Maombi yanatumwa kupitia ofisi za vijiji na kata kwa idara ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya wilaya. Wanawake wanaostahili ni wale wenye umri unaoanzia miaka 15 kwa sababu mara nyingi wasichana huanza kuzaa watoto katika umri huo. Masharti mengine ya kupata mkopo huo ni pamoja na:

- Kuwa kwenye kikundi cha watu watano ambacho kina katiba, lazima kiwe tayari kimeanzisha biashara fulani kabla ya kuomba mkopo, na kiweze kuwasilisha picha za kila mwanakikundi
- Kutumia muhtasari kutoka kwenye mkutano wa kijiji kama ushahidi, uthibitishwe na viongozi wa kijiji
- Kuwa wakazi wa kudumu wa eneo hilo na kuwa na mali zisizohamishika
- Uthibitisho kutoka Kamati ya Kata baada ya kupokea uthibitisho kutoka kwa viongozi wa kijiji, na muhtasari kutoka kwenye majadiliano ya mkutano/mikutano ya Kamati ya Kata uambatishwe kwenye maombi
- Fomu ya mkopo iliyojazwa na kulipiwa ada ya usajili

Changamoto kadhaa ziliripotiwa kuwa kikwazo kwa wanajamii wengi, hususan maskini, katika kupata mikopo ya halmashauri ya wilaya. Changamoto hizo ni pamoja na uhaba wa fedha za kuvipa vikundi vingi kwa sababu mfuko unategemea mapato ya halmashauri yaliyokusanywa, uelewa kwa watu wengi kuhusu upatikanaji wa fursa iliyopo, uelewa kuhusu faida za kujiunga na vikundi, na elimu ya ujasiriamali.

Mikopo binafsi

Katika maeneo yote matatu, wilaya ya Bukombe pekee ndiyo ilikuwa na taasisi ya mkopo binafsi: BRAC. Wafanyakazi wa BRAC walitembelea kijiji hicho na kuhamasisha wanajamii kuanzisha vikundi vya watu 15 ili waweze kupata mikopo ya BRAC yenye viwango vidogo vya riba. Mikopo ya BRAC

inalenga wanawake, na kila mwanamke katika jamii anaweza kupata mkopo maadam awe amekidhi vigezo:

- Uwe katika kikundi cha angalau watu 15, ingawa mikopo hutolewa kwa mtu mmoja mmoja kulingana na mahitaji yao
- Dhamana kutoka kwa watu wawili kwa kila mwanachama: mtu mmoja kutoka nje ya kikundi na mtu mwingine kutoka ndani ya kikundi
- Tamko la umiliki wa mali (k.m., nyumba, ardhi)
- Uwepo wa biashara, bila kujali ukubwa
- Ushiriki katika mafunzo yanayohusu usimamizi wa biashara na fedha

BRAC ni taasisi mpya sana (ina miezi mitatu). Washiriki walisema kwamba karibia watu 200 walionesha nia, lakini hadi sasa ni watu 15 tu ambao wameshapata mikopo, kwa sababu ya:

- Mlolongo kwa ajili ya vikundi kupata uthibitisho wa mikopo ni mrefu
- Uelewa mdogo kuhusu kwa nini watu wanapaswa kutangaza mali zao zisizohamishika wakati wa mchakato wa maombi
- Wanawake wengi wanasita kujiunga na vikundi ili kupata mikopo kwa kuogopa kufilisiwa
- Baadhi ya wanaume wanawakataza wake zao kujiunga na vikundi
- Kuenea kwa uvumi katika jamii na hofu kwamba fedha za BRAC zinahusishwa na "freemasons"

Vyama vya kuweka na kukopa vijijini (VLSA)

Katika kila wilaya, kuna Chama cha Kuweka na Kukopa (VSLA) kilichosajiliwa na kinafanya kazi na vikundi vingine vidogo vidogo vya kuweka akiba, kama vile VICOBA. Hata hivyo, uwepo wa vikundi hivi katika maeneo ya utafiti ni mdogo. Kwa mfano, hakukuwa na vikundi vya aina hiyo kule Kerezia (Bukombe), kulikuwa na kikundi kimoja tu huko Itumbi (Chunya), na angalau vikundi nane huko Saza (Songwe). Idadi rasmi ya Vikundi vya Kuweka na Kukopa (VSLAs) na vikundi vya VICOBA katika wilaya husika haikuweza kuthibitishwa kwa sababu taarifa hizi zinatunzwa kwenye makaratasi.

Sababu kuu iliyotolewa ya kiwango kidogo cha usajili wa vikundi vya Kuweka na Kukopa (VSLAs) na vikundi vya VICOBA katika jamii za utafiti ni kwamba wanajamii wengi hawajui faida ya kujiunga na vikundi ili kupata mikopo na elimu ndogo ya ujasiriamali na ubunifu wa biashara. Sababu nyingine ni pamoja na ujuzi mdogo au kutokuwa na ujuzi au uelewa wa kuanzisha na kuviendesha vikundi, usimamizi mbaya wa fedha, kipato kidogo/ukosefu wa fedha za kujiunga na vikundi, na ukosefu wa motisha.

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

TASAF ni moja ya mifuko ya hifadhi ya serikali kwa ajili ya kusaidia kaya maskini na zinazoishi katika mazingira hatarishi nchini. TASAF inatoa misaada ya kifedha, yote yenye masharti na isiyo na masharti (k.m., mpaka mtoto atakapohudhuria shule). Shughuli za TASAF zinatekelezwa katika kila wilaya za utafiti, lakini hakuna kijiji au kitongoji hata kimoja kilichohusika kwenye utafiti kilichokidhi vigezo kwa ajili ya kupata msaada wa TASAF.

3.14.4. Programu za ulinzi wa mtoto

Huko Geita, wilaya ya jirani ya Bukombe, shirika la Plan International limeshirikiana na mamlaka za wilaya na AZAKi, NELICO na CODERT kutekeleza mpango wa ulinzi wa mtoto unaowalenga Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini (CIM). Majadiliano na mratibu wa mpango huko Geita yalionesha kuwa mpango umefanikiwa kupunguza idadi ya watoto wanaofanya kazi katika migodi na kuwaunganisha watoto na huduma za kijamii, kama vile elimu na kuungana na familia zao tena. Baadhi ya shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na shughuli za kuimarisha uchumi, mafunzo ya ufundi kwa vijana, kutoa elimu kuhusu madhara ya kuwahusisha watoto katika shughuli za uchimbaji madini, namba ya simu ya bure kwa ajili ya kutoa taarifa za ajira za watoto na unyanyasaji, kusaidia mifumo ya ulinzi wa watoto ya kata na wilaya, na kuanzisha mabaraza ya kupaza sauti ya watoto ambapo watoto wanahimizwa kupaza sauti dhidi ya vitendo vyovyote vinavyohusiana na ajira za watoto kwenye migodi na unyanyasaji wa watoto.

Kwa kuzingatia mfanano wa hali ya kijamii na kiutamaduni miongoni mwa maeneo ya migodi, mradi wa USAID Kizazi Kipya unaweza kujifunza kutoka kwenye shughuli za Plan International ambazo tayari zinaonekana kuwa na mafanikio na kuzifanya ziweze kutekelezwa katika maeneo ya Kizazi Kipya.

4. Mapendekezo

Matokeo ya tathmini yalitumiwa katika hatua mbili ili kuelezea muundo wa utekelezaji. Hatua ya kwanza, matokeo ya utafiti yalijadiliwa na wadau wote wa Kizazi Kipya na washirika wa serikali tarehe 2 Agosti 2017. Hatua ya pili, wakati wa Majadiliano ya Kikundi (FGD), wanajamii waliombwa kutaja mikakati inayowezekana ya kuimarisha uchumi katika maeneo yao. Mapendekezo yafuatayo yalitoka kwenye mchakato huu.

4.1. Hatua ya 1: Mapendekezo ya utekelezaji

4.1.1. Jamii

- Washiriki walielezea haja ya kuanzisha programu za kujitambua ambazo zitawalenga wadau mbalimbali wa madini, watoto wenyewe, na jamii kwa ujumla juu ya madhara ya kuwashirikisha watoto katika shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini.
- Programu inapaswa kuwafanya watambue hatari za kiafya zinazohusiana na matumizi ya zebaki na asidi ya sulfuriki.
- Wanajamii wanapaswa kuhamasishwa kuwasaidia watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi zaidi kupata mahitaji ya msingi, kama vile kuanzisha Vikundi vya Kuweka na Kukopa (VSLAs) ambavyo vitatoa fedha kwa ajili ya mahitaji ya watoto.
- Wanajamii wanapaswa kuungwa mkono kuanzisha vituo vya kuhudumia watoto, na kina mama wanapaswa kuaswa kutoenda na watoto wao wadogo kwenye maeneo ya migodi.
- Kaya na vijana wadogo/wakubwa wanapaswa kuwezeshwa kuanzisha vyanzo mbadala vya mapato, kama vile biashara ndogondogo, shughuli za kilimo, na kufuga wanyama. Vijana wadogo na wakubwa wanapaswa kupata mafunzo stadi na mtaji wa kuanzia.
- Kushirikisha jamii katika kutunga na kutekeleza sheria za ajira za watoto. Hii inapaswa kuhusisha kufafanua hatua zitakazochukuliwa kwa mtu yeyote anayewashirikisha watoto katika shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini, ikiwa ni pamoja na waajiri, wazazi wa wachimbaji watoto, na wachimbaji watoto wenyewe.
- Kutoa namba ya bure au njia yoyote ya siri ya kutoa taarifa bila kutambuliwa kuhusu watoto wanaofanya shughuli zinazohusiana na uchimbaji madini au kufanyiwa vitendo vya unyanyasaji.
- Wazazi wanapaswa kuelimishwa na kujengewa uwezo ili kutekeleza sheria ya ndoa. Wazazi, hususan kina baba, wanatakiwa kuwajibika kwa watoto wao na familia zao. Pia, hatua madhubuti zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya wazazi/walezi wanaowaozesha watoto wao ambao hawajafikisha umri wa miaka 18, bila kujali hata kama mtoto mwenyewe anataka kuoelewa.
- Watoto na vijana wanapaswa kupewa msaada wa kisheria na gharama zinazohusiana.
- Wazazi wanapaswa kuhimizwa kuwapeleka watoto wao shule, kuwasaidia watoto kuendelea na shule, na kuhakikisha kwamba watoto walioandikishwa wanahitimu masomo yao kikamilifu.

4.1.2. Utoaji wa huduma

- Kuimarisha upatikanaji wa elimu endelevu ya afya kuhusu kinga na matibabu ya magonjwa ya kuambukiza, ikiwa ni pamoja na VVU na magonjwa mengine yanayoambukizwa kwa njia ya ngono, na kukabiliana hatari maalum za uchimbaji madini.
- Programu kama vile za usambazaji wa vyandarua pia zinapaswa kulenga jamii katika maeneo ya migodini, na maangalizo yanapaswa kuwepo ili kuboresha hali ya maji na usafi wa mazingira katika migodi.
- Kuendelea kutoa elimu ya kujitambua na kuhusu madhara ya matumizi ya zebaki na asidi ya sulfuriki.
- Utoaji wa huduma tembelezi za kupima VVU na utoaji ushauri nasaha, utoaji wa ART, na kuunganisha (elimu, usafiri, kuongozana, kufuatilia) ili kupata huduma za VVU zinapaswa kuimarishwa.
- Watoto wanapaswa kurudishwa tena kwenye mfumo rasmi wa elimu k.m., kwa kutumia Mfumo wa Shule. Kamati za maendeleo ya shule zinapaswa kujumuisha viongozi wa jamii, wadau wa madini na wazazi wa wachimbaji watoto.

- Mazingira ya shule yanapaswa kuvutia wanafunzi, kwa mfano kwa kuanzisha programu za michezo na kuimarisha mpango wa kutoa chakula shuleni, kuhamasisha na kuwavutia wanafunzi kuwa shuleni.

- Wahudumu wa afya ya jamii wanapaswa kuunganishwa ili kupata huduma za ulinzi na kufuatilia kesi za unyanyasaji, kufanyiwa kazi, na unyanyasaji wa watoto.
- Kuanzisha na/au kusaidia huduma za kisheria katika ngazi za wilaya na za mikoa

4.1.3. Sera

- Miongozo ya huduma za upimaji VVU na kutoa ushauri nasaha zinapaswa kuruhusu upimaji wa VVU kwa vijana wenye umri wa chini ya miaka 18 bila idhini ya mzazi/mlezi.

4.2. Hatua ya 2: Mapendekezo ya wazazi na wajumbe wa kamati ya maendeleo ya Kata kwa ajili ya shughuli za kuimarisha uchumi

Shughuli za kuimarisha uchumi zilizoonekana kuwa sahihi zaidi kwenye maeneo ya migodini zilikuwa ni kilimo cha kisasa; biashara ndogondogo na za kati, kama vile kununua na kuuza mazao; na mafunzo ya ufundi, hususan useremala, ufundi viatu, ushonaji, uashi, na umakanika, kama vile ufundi pikipiki. Ilielezwa kuwa mtaji wa kuanzia unapaswa kutolewa baada ya kuhitimu mafunzo ya ufundi, mikopo au mtaji wa kuanzia ili kuanzisha ufugaji wa kuku, na mafunzo ya ujasiriamali, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa fedha kwa ngazi za mtu binafsi na kaya. Jedwali la 3 linaelezea hii mikakati muhimu na ya nyongeza kwa ajili ya kupunguza idadi ya Watoto Walioko kwenye Machimbo ya Madini (CIM) na kuboresha afya kama ilivyopendekezwa na wazazi na viongozi wa jamii kwenye jamii za wachimbaji.

Jedwali la 3: Mikakati muhimu ya kupunguza ajira za watoto katika machimbo ya madini na kuboresha afya, kama ilivyoelezwa na wazazi na wanakamati ya maendeleo ya kata

Na	Mikakati	Vikwazo	Njia za kukabiliana na vikwazo
1	Utoaji wa mafunzo muhimu kuhusu kilimo cha kisasa ili kuongeza tija Kusaidia kaya kwa kutoa pembejeo za kilimo	• Idadi ndogo ya maafisa ugani wa kilimo • Uelewa mdogo kuhusu shughuli za kilimo cha kisasa • Kuchelewa kwa pembejeo za kilimo kutoka serikalini • Utegemezi mkubwa kwa serikali kwenye utoaji wa pembejeo za kilimo • Ukosefu wa mtaji wa kununulia pembejeo muhimu za kilimo na vifaa	• Serikali inapaswa kutoa pembejeo za kilimo kwa wakati. • Maafisa ugani wa kilimo wanapaswa kupewa vifaa muhimu vya kufanyia kazi. • Mashirika ya ndani, taasisi binafsi, na mashirika mengine yasiyo ya kiserikali wanapaswa kutoa mkopo mdogo ili kuwawezesha wakulima wadogo wadogo.
2	Utoaji wa mafunzo kuhusu kuunda na kusimamia Vikundi vya kuweka akiba na kukopa (VSLAs) Utoaji wa mafunzo ya ujasiriamali kwa Vikundi vya kuweka akiba na kukopa (VSLAs) ili kuwa na uwezo wa kusimamia biashara ndogo ndogo na shughuli zingine za kiuchumi	• Ukosefu wa ujuzi wa kitaalamu ili kuanzisha na kusimamia Vikundi vya Kuweka na Kukopa (VSLA) • Ukosefu wa elimu ya ujasiriamali • Mbinu duni za usimamizi wa fedha • Uelewa mdogo juu ya umuhimu wa kuunda vikundi • Ukosefu wa malengo ya pamoja miongoni mwa wanakikundi	• Kutuma wataalam kwa jamii ili kuwawezesha viongozi wa jamii, vikundi, na kaya kuanzisha na kusimamia Vikundi vya Kuweka na Kukopa (VSLA) na kutoa mafunzo ya ujasiriamali.
3	Utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa vikundi vilivyoanzishwa au kaya maskini	• Ukosefu wa mtaji wa kuanzisha biashara za mazao • Taasisi nyingi za kifedha zinalenga familia zenye kipato cha kati	• Serikali inapaswa kuhamasisha taasisi za fedha kupunguza vikwazo na masharti ili kupata mikopo, hususan kwa familia maskini.

Na	Mikakati	Vikwazo	Njia za kukabiliana na vikwazo
		• Taasisi zinaweka masharti magumu ambayo yanafanya kuwa vigumu kwa familia kupata mikopo	
4	Utoaji wa elimu kuhusu mbinu za malezi na hatari zinazohusiana na ushiriki wa watoto katika shughuli za uchimbaji madini	• Ukosefu wa wataalamu wa masuala yanayohusu mbinu za malezi • Ujuzi mdogo kuhusu hatari za kijamii na afya kwa Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini (CIM) • Ukosefu wa rasilimali fedha au viongozi wa kijiji kusaidia /kutoa elimu ya afya kwa jamii	• Taasisi binafsi /Mashirika yasiyo ya serikali na wilaya / jamii wanapaswa kuanzisha idara za kutoa elimu ya malezi kwa jamii za wachimbaji. • Taasisi binafsi / Mashirika yasiyo ya serikali, wilaya / jamii, na idara za ustawi wa jamii zinapaswa kutoa elimu juu ya hatari za kiafya na kijamii za Watoto walioko kwenye Machimbo ya Madini (CIM.)
5	Utoaji wa mafunzo ya ufundi, k.m., ushonaji, useremala, uashi, na umakanika / ufundi pikipiki, hususan kwa wale watoto ambao walimaliza elimu ya msingi lakini hawakufanikiwa kwenda shule ya sekondari	• Kukosekana kwa taasisi za mafunzo ya ufundi • Familia ambazo haziwezi kumudu kuwapeleka watoto wao kwenye taasisi za mafunzo ya ufundi mbali na wilaya wanayoishi	• Kuhimiza serikali na taasisi zingine binafsi kuanzisha taasisi za mafunzo ya ufundi ndani ya jamii za wachimba madini. • Kutoa msaada wa kifedha kwa wanafunzi kadhaa wanaotoka kwenye kaya maskini ili kupata mafunzo ya ufundi mbali na eneo la mgodi.
6	Utoaji wa mtaji wa kuanzia baada ya kuhitimu mafunzo ya ufundi	• Ukosefu wa mtaji wa kununulia vifaa vya kufanyia kazi baada ya kuhitimu mafunzo ya ufundi, kama vile vyerehani	• Kuwawezesha wale waliohitimu mafunzo yoyote ya ufundi kwa kuwapa mitaji ya kufungua biashara. • Kuhimiza watoto waliomaliza shule lakini hawakuendelea na masomo kuanzisha vikundi na kupata fedha ili kusaidia kuanzisha biashara
7	Utoaji wa huduma za afya na kijamii kwa jamii za wachimbaji, kama vile zahanati na shule za sekondari	• Hamna zahanati kwenye jamii • Umbali mrefu kwenda shule ya sekondari	• Viongozi wa mitaa wanapaswa kufanya harambee ya uchangishaji fedha kijijini na maeneo ya jirani kuchangia fedha na rasilimali zingine zinazohitajika ili kuanzisha ujenzi wa zahanati na shule. • Serikali na taasisi binafsi zinapaswa kutoa msaada. • Serikali za mitaa zinapaswa kujumisha zahanati na shule za sekondari kwenye bajeti na mipango yao.
8	Viongozi wa kijiji kuanzisha utungaji na usimamizi wa sheria ndogo Usimamizi wa sheria ndogo zilizopo zinakataza watoto kufanya kazi katika Mazingira Mabaya zaidi ya Ajira za watoto (WFCL), kama vile uchimbaji madini	• Sheria zilizopo hazisimamiwi kikamilifu na viongozi wa kijiji • Baadhi hawajui kama kuna sharia ndogo • Masuala ya kisiasa linapokuja suala la kusimamia sheria ndogo	• Kuwafanya wadau wote ikiwa ni pamoja na wanasiasa watambue sheria ndogo zilizopo na kuanzisha utaratibu wa kuzisimamia
9	Utoaji wa vifaa muhimu vya shule, kama vile penseli/kalamu, vitabu, sare za shule, na madaftari ya mazoezi	• Elimu inapewa kipaumbele kidogo na wazazi • Familia duni • Ukubwa wa familia/wazazi hawana uwezo wa kutoa mahitaji ya shule kwa watoto wote wanaosoma shule katika familia zao	• Wanajamii wanapaswa kuarifiwa kuhusu umuhimu wa elimu kwa watoto wao na kuhimizwa kuhakikisha kuwa wanahudhuria na kuhitimu/kumaliza shule.
10	Kufanya shule zivutie	• Ukosefu wa vifaa vya michezo • Ukosefu wa mashindano ya michezo	• Kuanzisha tuzo za michezo • Kutoa vifaa vya michezo shuleni
11	Utoaji wa elimu ya jinsia na afya ya uzazi	• Masuala ya kiutamaduni • Dhana potofu kuhusu hatari zinazotokana na matumizi ya njia za uzazi wa mpango	• Kuongeza utoaji wa elimu ya jinsia na afya ya uzazi hususani kuhusiana na uzazi wa mpango